

# Kesi

Topeka, Kansas, USA

Juni 21, 1964

1 Kwa ajili ya kusoma Maandiko, alasiri ya leo, kutoka kwenye Kitabu cha Marko, mlango wa 16 wa Marko. Nami nawatakeni msimame, pamoja na Biblia zenu, tunaposoma Neno la Mungu. Marko 16, kuanzia kifungu cha 9.

*Naye Yesu alipofufuka alfajiri siku ya kwanza ya juma, alimtokea kwanza Mariamu Magdalene, ambaye kwamba alimtoa pepo saba.*

*Huyo akashika njia akawapasha habari wale waliokuwa pamoja naye, nao wakali wanaomboleza na kulia.*

*Walakini hao waliposikia kama yu hai, naye amemwona, hawakusadiki.*

*Baada ya hayo akawatokea kwa sura nyingine, wawili...(Samahani.)*

*Baada ya hayo akawatokea watu wawili miongoni mwao, ana sura nyingine; nao walikuwa wakishika njia kwenda shamba.*

*Na hao wakaenda zao wakawapasha habari wale wengine; wala hao hawakusadiki...*

*Baadaye, akaonekana na wale kumi na mmoja walipokuwa wakila, akawakemea kwa kutokuamini kwao na ugumu wa mioyo yao, kwa kuwa hawakuwasadiki wale waliomwona alipofufuka katika wafu.*

2 Hiyo si ni picha ya siku hizi! Hawaamini wewe ni shahidi wa jambo hilo.

*Akawaambia, Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe.*

*Yeye aaminiye na kubatizwa ataokoka; bali yeye asiyeamini atahukumiwa.*

Hilo linafanya tu mstari, upande mmoja ama mwingine.

*Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; Kwa jina langu watatoa pepo; watanena kwa lugha mpya;*

*Watashika nyoka; na wakinywa kitu cha kufisha, hakitawadhuru; wataweka mikono yao juu ya wagonjwa, ... watapata afya.*

*Basi Bwana, baada ya kusema nao, akachukuliwa juu mbinguni, akaketi mkono wa kuume wa Mungu.*

*Nao wale wakatoka,...wakahubiri kotekote. Bwana akitenda kazi pamoja nao,... kulithibitisha lile neno kwa ishara zilizofuatana nalo. Amina.*

Na tuinamishe vichwa vyetu.

3 Bwana, tunaamini hili kuwa ndilo agizo la mwisho kwa kanisa. Tunaamini ya kwamba Neno lilifanyika mwili likakaa kwetu. Nasi tunaamini ya kwamba mtu ye yote si bora kuliko neno lake, kwa hiyo tunaamini ya kwamba Neno hili ni Wewe. Nasi tunaamini ya kwamba ni Wewe, ambapo, ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Njoo, leo, Ee Baba Mungu, katika umbo la Neno, kwetu, na uwajalie watu waone ya kwamba Wewe Ndiye Kristo aliyefufuka, na umefufuka katika siku hii ya mwisho, katika umbo ulilosema ungekuwa ndani yake, Neno lililodhihirishwa. Ulipokuwa duniani, Wewe ulikuwa Ndiye Neno lililotabiriwa, lililodhihirishwa katika umbo la mwanadamu. Nalo Neno limetabiriwa kwa ajili ya siku hii. Njoo, Bwana Yesu, na utuletee, leo, Neno. Fanya tafsiri Yako ya Neno, tupate kuwa na "furaha isiyoelezeka, na iliyojaa utukufu." Hata tumekuona unapendeza, na kuona Maneno Yako ni kweli na kuthibitishwa mioyoni mwetu, ya kwamba tumepita kutoka mautini kuingia Uzimani.

Sisi sote tuliozaliwa na huo mti mmoja katika bustani ya Edeni, ambao ulikatazwa kuguswa, mwanamke, kwa kuwa ndani yake hamna uhai; yeye ni yai tu. Uhai huo ulitoka kwa yule Mtu, ambaye alikuwa ni Kristo. Nasi tumezaliwa na mwanamke, na, kama Biblia inavyotwambia, "wa siku chache, na zimejaa huzuni na taabu."

4 Baba, pia tumezaliwa na Yule atoaye Uzima, kutoka kwa Mwanadamu. Mtu mume humjia mtu mke, nayo chembe hai inatokana na mume; kama vile Roho Wako alivyomtia uvuli yule bikira, na ndani ya tumbo lake la uzazi ikaumbwa chembechembe ya Damu; hiyo chembechembe ya Damu, si ya Kiyahudi, si ya Kimataifa, bali ni ya Mungu, Damu iliyumbwa. Katika Damu hiyo, tuna matumaini yetu. Haikuwa ni ya mwanamke, wala ya mwanamume; ilikuwa ni ya Mungu.

Kwa hiyo tunaomba leo hii, Bwana, kwa kuwa tumejiona wenyewe ni washiriki wa ule mti-mwanamke, nasi sote hatuna budi kufa kwa sababu hamna uhai katika mwanamke, sasa pia, Baba, tumepewa

majaliwa ya kushiriki kwenye ule Mti-Mume, ambao ni Kristo. Na sasa, kupitia Yeye, tunao Uzima, Uzima, lile Neno, limekuwa Uzima miongoni mwetu. Tujalie, Bwana, ya kwamba mambo haya yatakuwa halisi sana kwa Kanisa, hata wataona, nasi tutafahamu ile saa tunayoishi.

Waponye wagonjwa na wanaoteseka. Jalia kusiwe na mtu mnyonge miongoni mwetu, alasiri ya leo, wakati ibada hii itakapofungwa. Jalia ikumbukwe kwa muda mrefu miongoni mwa watu! Wajalie watumishi Wako, wa—wachungaji, wachunga kondoo, jalia wavuviwe sana mpaka makanisa yao yatafanyiwa mapinduzi na ibada kuu zifanyike, na waanzishe uamsho wa mtindo wa kale mumu humu katika mji huu, miongoni mwao, ambao utaenea kote jimboni na nchini, na hata kote ulimwenguni. Jalia hilo, Bwana. Wewe umeshika funguo za maombi haya mkononi Mwako. Tusaidie, tunaomba, katika Jina la Yesu. Amina.

Mnaweza kuketi.

5 Mungu hana budi kuleta hukumu juu ya nchi. Naye Mungu hana budi kuwa na kitu fulani hapa, kigezo, kuuhukumia ulimwengu, kwa maana ingekuwa si haki, katika Mungu, kuuhukumu ulimwengu, huku ulimwengu haujui kigezo cha kutumia. Ni wangapi wanaoamini hiyo ni kweli? Kama kanisa ndilo kipimo, ni lipi? Neno, Mungu alisema angeuhukumu ulimwengu kwa Yesu Kristo. Yeye ni Neno. "Hapo mwanzo kulikuwako Neno, Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Neno alifanyika mwili akakaa kwetu." "Yeye yule jana, leo, na hata milele."

6 Sasa ninataka kunena nanyi alasiri ya leo juu ya somo la kigeni sana, huenda likawa hivyo kwenu. Lakini, katika somo hili, nitampa Bwana wangu jaribio la—la haki. Sidhani alipata kesi ya haki mbele ya mahakama ya Pilato. Si—siamini alikuwa na—alikuwa na kesi ya haki, kwa hiyo walimpata na hatia, na wakamhukumu na kumsulibisha. Lakini tutachukua hatua, alasiri ya leo, kama katika kesi hii.

Nanyi mnasema, "Ati ungeweza kumfanyia kesi?"

Kama Yeye anadumu akiwa ni Neno, tunaweza kumfanyia kesi, kwa kuwa Yeye angali ni Neno. Nasi tunaweza kumfanyia kesi. Nami ninataka kuona hilo katika mahakama hii, alasiri ya leo, tunapolichukua jengo hili kuwakilisha mahakama, ambapo tunataka kuhakikisha ya kwamba Yeye anapata kesi ya haki, kama ni wanaomtetea ama wanaomshtaki. Tunataka kutoa pande zote mbili. Halafu basi, katika kesi hii, ninataka kuisikiliza kesi Yake, ambaye ni Neno.

7 Sasa, haya Maandiko ambayo ndiyo kwanza nisome, Marko mlango wa 16, hata Daktari Scofield hapa anasema, "Kutoka kifungu cha 9 na kuendelea, hayapatikani katika magombo mawili yaliyo ya kale zaidi." Inaaminiwa sana miongoni mwa watu, ya kwamba, walimu wetu wa siku hizi wanaotaka kuliadini namna hiyo, ya kwamba yameingizwa mle na Vatikani.

Lakini ninaona ya kwamba Ireneo na wengi wa waandishi wa mwanzoni wanarejea kwenye Marko 16. Kama vile ninyi watu wengine mnaosoma historia, historia ya Biblia, mnavyojua ya kwamba hao mitume wa mwanzoni, na hata baada ya kifo cha Yesu, na wakati Polycarp, na Ireneo, na Mtakatifu Martin, na Mtakatifu Columba, na hao wote, walirejea kwenye Marko 16. Kwa hiyo halina budi kuwa ni la kweli, la sivyo wasingalirejea kamwe. Naye Yohana Mtakatifu ndiye aliyeziweka zile nyaraka pamoja, naye Polycarp alikuwa rafiki msiri na alimsadia kufanya hivyo, kulingana na historia.

Sasa tunaona ya kwamba leo hawaamini jambo hilo. Wanajaribu kuuondokea uhalisi wa Mungu kuwa ni halisi; badala yake, azimio tu ama kanuni za imani. Mungu aliye halisi, mlango huu ungethibitisha kwamba ni halisi, na thibitisho lolote wanaloweza kulipata.

8 Kama vile mwalimu fulani mashuhuri sana, rais wa Misheni za Sudan, maskini mke wangu pale alikuwapo wakati alipokuja nyumbani kwangu, Paris Reidhead. Naye akasema, "Ndugu Branham, nasikia ya kwamba ulikuwa Mbatisti."

Nikasema, "Naam, bwana, hiyo ni kweli."

Naye akasema, "Vema," kasema, "nataka kukuuliza jambo fulani." Akasema, "Nilipokuwa mvulana mdogo," kasema, "nilipata tukio. Naye mama yangu alifua na kila kitu, apate kunipeleka shuleni. Nami nikawazia, hakika, ya kwamba nitakapopata B.A. yangu, ya kwamba nitampata Kristo." Akasema, "Hiyo, wakati nilipokabidhiwa hiyo, sikumpata. Nilipopata Digrii yangu ya Udaktari, nilifikiri ningempata. Nilipopata LLD yangu, nilifikiri ningempata." Akasema, "Ndugu Branham, ninazo digrii za kutosha, za kawaida na—za kawaida na za heshima pia, hata ningeweza kukandika kuta zako kwazo. Lakini yuko wapi Mungu wa Biblia?" Akasema, "Walimu walikosea?"

Nikasema, "Mimi ni nani kusema ya kwamba waalimu walikosea?"

9 Akasema, "Vema, hivi ndivyo ninavyosikia, ya kwamba uligeuka ukawa Mpentekoste."

Nami nikasema, "Vema, sisemi mimi ... Ninaamini, nilipozaliwa katika Ufalme wa Mungu, moja kwa moja nilikuwa mpentekoste," nikasema, "kwa sababu pentekoste si dhehebu. Wamejaribu kuifanya hivyo, bali sivyo ilivyo. Mungu atamjaza Mpresbiteri, Mluteri, ama ye yote yule. Mnaona, kwa hiyo ni tukio na si

dhehebu. Huwezi kuiundia dhehebu. Ni tukio.”

Naye akasema, “Vema, ninataka kukwambia kilichotukia.” Akasema, “Kutoka India, siku hizi, wanawatuma watu huku wapate elimu yao.” Kasema, “Katika shule yetu, kulikuwa na mvulana mzuri wa Kihindi aliyekuja hapa naye akapata elimu. Na aliporudi ...” Nafikiri alikuwa awe, nadhani, mhandisi wa umeme ama cho chote kile. Yeye alisema, “Lakini wakati sisi ...”

10 Wanayo shule kama tu Ndugu Oral Roberts alivyo nayo kule. Wanafundisha uhandisi na chochote kile.

Kwa hiyo akasema, “Alipokuwa akirudi, mimi pamoja na mhudumu mwingine, tulimwambia, 'Sasa, unarudi India...'" Nanyi mnajua Wa—Wahindi wanamwabudu Mohammed. Basi akasema, “Kwa nini usimwache maskini nabii wako wa kale aliyekufa, na kumpokea Bwana Yesu aliyefufuka; nawe urudi India pamoja na Mungu aliye halisi, ukawaambie watu wako?”

Akasema, “Bwana,” akasema, “Bwana wako Yesu angeweza kunifanyia nini zaidi ya vile nabii wangu anavyoweza kufanya?”

Naye akasema, “Vema, Bwana wangu Yesu anaweza kukupa Uzima wa Milele. Ni ahadi katika Neno.”

Yeye alisema, “Nabii wangu, Mohammed, aliahidi jambo lile lile, katika neno lake.”

Naye akasema, “Vema, unaona,” akasema, “Bwana wangu Yesu amefufuka katika wafu. Nabii wako yuko kaburini.”

Yeye alisema, “Je! Yeye alifufuka katika wafu?” Kasema, “Umekuwa na miaka elfu mbili kuthibitisha jambo hilo, na asilimia themanini ya ulimwengu hawajapata kusikia habari zake.” Yeye alisema, “Hebu Mohammed afufuke katika wafu, na ulimwengu wote utajua, katika muda wa saa ishirini na nne.”

11 Sasa, yeye alisema, “Vema, angalia,” akasema, “Yesu amefufuka katika wafu.” Kasema, “Ninaweza kuthibitisha jambo hilo kwa sababu Yeye anaishi ndani ya moyo wangu,” alisema Mkristo huyo.

Ndipo yule Mwislamu akasema, “Na, bwana, Mohammed anaishi moyoni mwangu.”

Yeye alisema, “Lakini, unaona, tuna nguvu na furaha.”

Akasema, “Bwana, dini ya Uislamu inaweza kutoa saikolojia nyingi tu kadiri Ukristo unavyoweza.” Na hiyo ni kweli.

Nimewaona wakilala mtaani na kusema kwa sauti kuu, “Allah,” na kuingia katika hali fulani, wangeweza kuchukua... Mimi na Billy tulisimama tukamwalia mtu akiuchomeka upanga moja kwa moja chini ya moyo wake; naye daktari akaenda pale na kumwaga maji kupitia hapo, yakatokea upande mwingine; akauchomoa, wala haukumdhuru. Tukawaona wakichukua vijbanzi, na kuviweka chini ya makucha yao ya vidole na kuyatoboa, na kuchoma ndoana kupitia puani mwao, na kamwe hawakuhisi wala kutoa tone la damu. Wanaweza kutoa saikolojia nyingi zaidi kuliko Ukristo unavyoweza.

Naye Bw.Redhead akaniambia, kasema, “Nilijua sikuwa nikizungumza na mshamba. Naye akasema, 'Sisi Waislamu tunangojea.'”

12 Kama walivyomfanyia ndugu yetu shujaa, Billy Graham, mliisoma gazetini, wakati Mwislamu alipomjia Bw. Graham, na kusema, “Wewe wachukue watu thelathini wagonjwa, nami nitawachukua watu thelathini wagonjwa; nawe hebu uwaponye hao thelathini wako, nami nitawaponya wangu thelathini kwa Muhammed,” mnaona, Bw. Graham akatoweka. Asingemjibu.

Siamini ningelifanya hivyo. Ningalikuwa kama wale wana wa Kiebrania, “Mungu wetu anaweza kutukomboza na jambo hili.” Kwa nini hakutuma, akamlete Oral Roberts ama mtu fulani? Kama hakuamini Hilo, aagize aletewe mtu fulani anayeliamini. Lakini, mnaona, kwa madhehebu, loo, wangemtupa nje papo hapo. Yeye ana kazi ya kufanya.

13 Hata hivyo, basi akasema, “Wakati sisi, huko India, tutakapowaona ninyi—ninyi Wakristo mkifanya kile Yesu alisema mngefanya,” kasema, “basi tutawaamini.” Akasema, “Yeye alisema alifufuka katika wafu, nao watu wangejua hilo kwa sababu mngefanya kazi zile zile alizofanya.”

“Vema,” akasema, “tunafanya kazi kubwa zaidi.”

Akasema, “Kamwe sikusema 'kubwa zaidi.' Ninataka tu kuona kazi alizofanya Yeye, kwanza.” Mbona, unazungumza, unajua huzungumzi na jamaa mdogo huko pembeni, wakati unapozungumza na mmoja wa hao wanatheo-...hao pamoja na theolojia yao. Kwa hiyo akasema, “Tunataka kuona kazi alizofanya.”

“Loo,” akasema, “labda unarejea kwenye Marko 16?”

Akasema, “Naam, bwana. Hiyo ni mojawapo, agizo Lake la mwisho kwa kanisa.”

Akasema, "Vema, sasa, unaona," kasema, "watu wengi wanaamini mlango huo kiulokole." Akasema, "Lakini tulijifunza, wasomi bora shuleni, ya kwamba Marko 16, kutoka kifungu cha 9 na kuendelea, kweli haujavuviwa."

Akasema, "Mbona, Bw. Reidhead!" Yeye alisema, "Ni sehemu gani iliyovuviwa basi?" Yeye alisema, "Labda zingine zote hazijavuviwa. Korani yote imevuviwa. Mnasoma kitabu cha namna gani, kinachoitwa Biblia?"

Akasema, "Nimeamua moyoni mwangu nitakuja kuzungumza na wewe. Naam, nilikuwa nizungumze na wewe."

Haya basi. Kama *Huu* haujavuviwa, basi vipi kuhusu mingine yote?

14 Inanikumbusha juu ya mama mmoja huko Chicago. Mvulana wake alienda kwenye seminari, kujifunza kuwa mhudumu, shule fulani ya Biblia na seminari. Na wakati alipokuwa hayuko, mama huyo mzee aliugua sana. Na kwa hiyo wakatuma taarifa kwa mvulana huyo 'akae chonjo,' mama yake ana homa kali sana, alikuwa na nimonia, na ikasema kwamba (mama) hu—huenda ikawa ni wito wa dharura. Kwa hiyo mvulana huyo akapanga nguo zake na akawa tayari. Hatimaye, kesho yake, hakusikia neno usiku kucha, na kesho yake, kasema, "Mambo yote ni shwari."

Kwa hiyo yapata mwaka mmoja baadaye, alirudi kutoka shule ya Mashariki, shule kubwa ya ualimu. Basi akaja nyumbani na kumwamkia mama yake wa thamani, na kusema, baada ya kuzungumza kwa muda kidogo, kasema, "Mama, kamwe sikupata nafasi ya kukuuliza ilikuwaje." Kasema, "Usiku mmoja waliniambia 'nikae chonjo', na kesho yake asubuhi, wakasema ulikuwa 'mzima.'" Kasema, "Daktari alitumia dawa gani?"

Kasema, "Mpenzi, daktari hakutumia kitu."

Akasema, "Vema, ulifanyaje jambo hilo?"

Kasema, "Je! unajua mahali ile misheni ndogo ilipo hapa chini kwenye...karibu na ule mzingo, pale katikati ya mji?"

"Naam."

Kasema, "Kulikuwako na mama. Walikuwa na mkutano wa maombi kule chini, usiku mmoja, kwenye misheni hii ndogo, maskini kundi hilo dogo nyenyekevu la watu, na," kasema, "mmoja wao alivuviwa kuja huku na kuniona. Ndipo wanawake wawili wakaja, nao wakaniuliza kama wangeweza kumleta mchungaji wao huku na—na kuniombea, na kunitia mafuta, na—na," kasema, "na kuniwekea mikono yao, nipate kuwa mzima." Kisha akasema, "Unajua, niliwaambia 'hakika.' Nao wakamleta mchungaji, naye akaweka mikono yake juu yangu, na kuomba." Kisha akasema, "Mpenzi, alisoma moja kwa moja kutoka katika Biblia, Marko sura ya 16, kasema, 'Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.'" Kisha akasema, "Unajua nini? Kesho yake asubuhi, daktari alikanganyika sana, hakujua la kufanya. Hakukuwa na homa ndani yangu."

15 "Loo," akasema, "mama, hukujihusisha na kundi hilo, sivyo?" Kasema, "Mnaona," akasema, "sisi shuleni, tulijifunza kwamba Marko 16, kuanzia kifungu cha 9 na kuendelea, haijavuviwa."

Akasema, "Utukufu kwa Mungu!"

"Mbona," akasema, "mama, unanza kutenda kama watu hao."

Akasema, "Nilikuwa nikiwazia tu jambo fulani." Kasema, "Nimekuwa nikisoma Biblia, kote kote, na ahadi zingine katika mahali pengine, pia, sawa na hiyo." Kisha kasema, "Nilikuwa tu nikiwaza, kama Mungu angeweza kuniponya kwa lile lisilovuviwa, angefanyaje na lile ambalo kweli limevuviwa?" Hiyo ni kweli.

Kwangu mimi, yote yamevuviwa. Mungu, nipe imani ya kuliadini na kulithibitisha!

16 Sasa tutabadilisha sasa, kwa dakika chache tu, za kesi mahakamani. Sasa, kumbukeni, tunaingia ndani ya chumba cha mahakama, kumleta Yesu, Mungu, jukwaani hapa, na kumfanyia kesi ya haki. Yeye angali ni Neno, hata la siku hizi, (mnaamini?), Kama tu vile alivyokuwa Neno wakati huo. [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.]

Sasa, kisa hiki, sababu yake, ni—ni Neno la ahadi za Mungu dhidi ya ulimwengu. Sasa fahamu mandhari yake vizuri kabisa la sivyo kamwe hutalipata. Sababu ya shtaka hili, ni kukiuka ahadi, "Mungu hatimizi Neno Lake." Ni kukiuka ahadi. Unajua ni kitu gani.

17 Sasa, daima tunaona ya kwamba wakili wa mashtaka hana budi kuwakilisha serikali, naamini hiyo ni kweli, mwendesha mashtaka. Kama kuna wakili anayeketi hapa, natumaini nimelipata hili vizuri. Wakili wa mashtaka hana budi kuwakilisha serikali. Kwa hiyo mwendesha mashtaka katika kesi hii ni ibilisi, akilishtaki Neno la Mungu.

Mshtakiwa wa Neno hili, ni Mungu Mwenyewe, kwa sababu Yeye ni Neno.

Shahidi wa Utetezi, katika kisa hiki, ni Roho Mtakatifu.

Na mw—mwendesha mashtaka ana mashahidi hapa alasiri ya leo. Na mashahidi hawa, mmoja wao, ni Bw. Asiyeamini, anayefuata ni Bw. Mwenye Kushuku, na mwingine ni Bw. Mkosa Subira. Wataletwa jukwaani, na kuapishwa, na kujaribiwa.

18 Sasa mna picha ya jinsi mahakama ilivyo, Mungu ameshtakiwa na ulimwengu, kwa sababu, ati “Yeye halitimizi Neno Lake.” Na mwendesha mashtaka anaiwakilisha serikali, ambayo inawakilisha ulimwengu. Naye mwendesha mashtaka ni ibilisi, anayekataa kwamba Neno ni kweli.

Na mwendesha mashtaka, kwa ajili ya mashahidi wake, analeta mashahidi watatu dhidi ya Neno la Mungu. Na kulithibitisha, yeye atawathibitishia jambo hilo, alasiri ya leo, ya kwamba, “Mungu halitii Neno Lake, wala ha—halipaswi kucheze. Si kweli kabisa. Halina ukweli wo wotei.”

Naye Mshtakiwa ni Mungu, ambaye ndiye Mwandishi na Neno, kwa ajili ya siku hii, sawa na siku hiyo au siku nyingine yoyote.

Na mwendesha mashtaka ana mashahidi wake.

19 Sasa unasema, “Wako wapi wazee wa mahakama?” Ninazungumza nao. Ninyi ndio wazee wa mahakama, na pia ninyi ndinyi hakimu. Sasa kumbukeni jambo hilo akilini, ninyi ni wazee wa mahakama na hakimu, kwenye kesi hiyo. Mimi ni msemaji tu.

Sasa mahakama iko tayari. Sasa kuweka nidhamu kunafanywa na wakili wa mashtaka. Amri inaitwa katika chumba cha mahakama, alasiri ya leo, kuleta kesi hii kwenye—shindano la kuamua.

Sasa watu wengi wamewaambia ya kwamba, “Neno la Mungu haliaminiki. Huwezi kulitegemea,” na kadhalika, naye umesikia haya yote. Sasa hebu na tulilete kwenye kesi ya kweli. Ni wangapi walio tayari, inua mkono wako na kusema, “Ningependa kusikia; na Yesu Kristo, ambaye ni Neno, afanyiwe kesi ya haki”? Na katika mahakama yetu, alasiri ya leo, tutamshtaki kwa haki. Acha tu adui achukue maneno ya adui, na lolote analotaka kusema, nasi tuone kama ni kweli. Hebu na tulichimbue na kumpa Yesu Kristo, Neno, kesi ya haki alasiri ya leo.

20 Sasa, mahakama inaamrisha utaratibu, shahidi wa kwanza ambaye mwendesha mashtaka anataka kumleta kizimbani ni...kizimbani ni Bw. Asiyeamini. Yeye anachukua msimamo kushuhudia. Sasa kumbuka, Bw. Asiyeamini. Usikose wahusika hawa sasa, ama utakosa kitu fulani, huenda ukakosa uponyaji wako.

Bw. Asiyeamini anakuja kizimbani, kutoa ushahidi. Malalamiko yake ni, kwamba, “Neno lote la Mungu la ahadi si kweli. Si kweli.” Anadai ya kwamba, katika Marko 16, ilihudumiwa kwake—kwake katika wanaouita mkutano wa Roho Mtakatifu. Naye alikuwa na ugonjwa wa tumbo kwa miaka kadhaa, naye akaenda mahali walipokuwa, kile wanachokiita, “mkutano wa Roho Mtakatifu,” naye alikuwa akiamini ya kwamba ahadi hii ya Marko 16 ilikuwa ni kweli. Alikuwa amewekewa mikono kulingana na ahadi ya Mungu.

21 Hana neno dhidi ya huyo mhudumu; alilisoma mumo humo kutoka kwa Neno. Yeye hamshtaki mhudumu; anamshtaki Mungu. Kwa sababu, si kosa la mhudumu, mhudumu anasoma tu yale Mungu aliyosema afanye. Na Mungu alisema kweli, katika Marko 16, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya.”

Naye anasema yeye ni mwaminio, naye alikuja kwenye mkutano kama huo ambapo walikuwa wakihubiri kwamba Marko 16 ni ya kweli. Naye mhudumu, mwenye Ubatizo wa Roho Mtakatifu, alidai ni mwaminio na ni mhudumu aliyetumwa kwa ajili ya kazi hiyo, alimwekea mikono yake. Na hiyo imekuwa miezi miwili iliyopita, na tumbo lake ni baya sana kama lilivyowahi kuwa. Kwa hiyo, anadai ya kwamba Mungu si mwenye haki, kuweka kitu kama hicho katika Neno, wakati si kweli.

Sasa hebu na ashuke. Yeye alitoa ushahidi.

22 Anayefuata kizimbani ni Bw. Mwenye Kushuku. Anataka kutoa ushahidi. Bw. Mwenye Kushuku anasema alikuwa amesumbuliwa na—na TB, kwa yapata miaka kumi na mitano. Lakini hakupona kabisa bado, iliendelea kuibuka tu, ika—ikazidi tu kuenea. Angepata nafuu kidogo tu, kisha aendele. Ndipo akasikia mahali fulani mjini ambapo palidhaniwa pana mhubiri mtauwa anayehubiri, nao watu walikuwa wakidai kuponywa kulingana na ahadi kutoka kwa Mungu, inayopatikana katika Yakobo 5:14, ambapo katika Neno la Mungu inasema, “Kukiwapo na mtu wa kwenu ambaye hawezi, na awaite wazee wa kanisa; nao wawapake mafuta na kuwaomba; kule kuomba kwa imani kutamwoko mgonjwa yule, Naye Mungu atawainua.”

Naye akiwa mgonjwa, na ni mwaminio, huenda kwenye mkutano huu ambapo watu hawa wote wanadai ya kwamba walikuwa wakiponywa na mchungaji huyu mcha Mungu. Naye alihudumiwa, kulingana na Yakobo 5:14. Naye mchungaji huyo akamhudumia kulingana tu na Neno, akampaka mafuta na

kumwombea, maombi ambayo mchungaji alisema yalikuwa ni "maombi ya imani," ambayo aliamini. Na hiyo imekuwa ni karibu mwaka mmoja uliopita, wala hajapata nafuu hata kidogo kutokana nayo, kwa hiyo Bw. Mwenye Kushuku anadai ya kwamba Mungu hana haki ya kuweka ahadi kama hiyo katika Biblia halafu ashindwe kusimama nyuma yake.

Sasa, kumbukeni, ninasoma ahadi zote za Injili hapa.

23 Shahidi anayefuata atakuja kizimbani sasa. Mwendesha mashtaka anamwita shahidi wake anayefuata, kabla hajaikamilisha kesi yake Shahidi wake anayefuata ni Bw. Mkosa Subira.

Sasa hizi ni tabia za ulimwengu wa roho zinazoishi ndani ya watu. Mnaona, sasa, huishi.

Kwa hiyo Bw. Mkosa Subira anakuja, naye anadai ya kwamba siku moja alikuwa akisoma katika Biblia. Hakwenda makanisani, bali alikuwa...alikuwa ni mwaminio. Kwa hiyo mmoja wao alimwendea mwinjilisti fulani, na huyo mwingine akaenda kwa mchungaji, naye jamaa huyu alikuwa tu ni mwaminio wa siri aliyekaa nyumbani. Naye akaenda na alikuwa akisoma katika Marko sura ya 11, aya ya 22 na 23; kama unaandika Maandiko hayo. Ambapo, Yesu Mwenyewe, akidai kwamba Yeye ni Mungu, Imanueli, alitoa tamshi hili kwa midomo Yake Mwenyewe, "Amin, amin, nawaambia, mtu atakayeuambia mlima huu, 'Ng'oka,' wala usitilie shaka moyoni mwako, bali uamini ya kwamba ulilosema litatimia, litakuwa lako." Na alisema pia, ya kwamba, "Mwombapo, aminini mtapokea mlichoomba, nanyi mtapewa."

24 Anasema amekuwa kilema miguuni mwake, kwa yapata miaka ishirini na mitano. Na miaka mitano iliyopita, alipokuwa ameketi chumbani, akijisikia ya kwamba alikuwa amevuviwa kusoma Neno ambalo anadai aliamini, na kwa moyo wake wote aliliamini. Ndipo basi akasema, kwa sauti yake mwenyewe, "Ulemavu miguuni mwangu, katika Jina la Yesu Kristo, niache," akasema. Na hiyo imekuwa ni miaka mitano iliyopita, naye ni kiwete tu kama alivyowahi kuwa.

Kwa hiyo, basi, Bw. Mkosa Subira anataka kuweka ushuhuda wake dhidi ya Neno kuwa lililoweza kukosea, anataka kuuweka dhidi ya Biblia kuwa ni Neno lililovuviwa, naye anasema ya kwamba ahadi hii si kweli; ameijaribu, nayo "Haikuwa ni ya kweli." Bw. Mwenye Kushuku alisema alijaribu, na "Haikuwa ni kweli." Bw. Asiyeamini alisema alijaribu, na "Haikuwa ni kweli." Mashahidi hawa wote watatu wanatoa masomo ya Kimaandiko, ahadi za Kimaandiko, na kusema ya kwamba ahadi hii inasema hivi, unaweza kuisoma katika Biblia, nao ni mashahidi ya kwamba "Si Kweli."

Kwa hiyo, Biblia inapaswa kutupiliwa mbali; maana, kama sehemu Yake moja, kifungu Chake kimoja hakiwezi kuaminiwa, nisingeweza kuamini sehemu Yake yoyote. Inapaswa kuwa yote ni Kweli, ama hakuna hata moja Yake iliyo Kweli. Mnyororo huwa ni imara tu kadiri kiungo chake kilicho dhaifu kuliko vyote kilivyo. Mnajua ninalomaanisha.

25 Sasa mwendesha mashtaka anakuja kuleta mashtaka na kuikamilisha kesi yake. Anataka kuikamilisha. Sasa angalia yale anayosema. "Mungu hana haki ya kuweka ahadi za kijinga kama hizo katika Neno Lake, kwa ajili ya watoto Wake wanaoamini kuijaribu imani yao kwazo, kwa kuwa si za kweli." Anao mashahidi hapa, kuthibitisha ya kwamba Neno hili ambalo Mungu ameahidi katika Neno Lake kuwa ni Kweli, anao mashahidi wanaoketi hapa, naye unaweza kuonyesha kwa thibitisho la daktari na kutoa ushahidi, ya kwamba wamekuwa wagonjwa, wamekuwa *hiki*, wamekuwa *kile*. "Nao wameyakubali haya Maandiko ya Kiungu, yanayosemekana yamevuvuwa, na kuyajaribu, nayo si ya kweli." Yeye ana mashahidi wa kuthibitisha hilo, kwamba, "Maneno haya si ya kweli, kwa kuwa Yeye alishindwa katika kila moja ya hayo hapo."

26 Sasa, sasa angalia tena. "Naye akashindwa. "Naye alishindwa. Mungu alishindwa kuwafanya hawa waaminio, ambao waliliamini Neno Lake, wakalichukua vivyo hivyo hasa, wakapitia kwenye utaratibu, vile vile hasa Yeye alivyosema, halafu Mungu hakusogeza kidole kamwe kufanya lolote kuhusu ahadi Yake; miaka na miaka imepita." Ndipo akasema, "Vipi kama Maandiko hayo mengine, kama vile kubatizwa, 'aaminiye na kubatizwa ataokoka,' halafu hakuna mtu yeyote anayeokolewa? Vipi kuhusu Maandiko haya yaliyoahidi ya kwamba Yeye atarudi? Hakuna hata moja la hayo lililo sahihi. Kwa sababu, *haya* si ya kweli, na *lile* si la kweli. Ni Kitabu tu cha hadithi za kubuniwa. Na watu hawa ni waaminio. Hata hivyo, Yeye, Mungu, anaahidi ya kwamba mambo yote yanawezekana kwa waaminio, nao hawa ni waaminio.

27 "Hata hivyo, tena, Yeye anadai kuwa yu hai baada ya kusulubishwa Kwake. Biblia inasema, ya kwamba, 'Yeye amefufuka katika wafu, na anabaki yeye yule jana, leo, na hata milele.' Na hakuna mtu aliyemwona Mtu huyu mwenye makovu ya misumari mikononi Mwake, akitembea miongoni mwa kanisa, na kadhalika. Na Waebrania 13:8 sivyo ilivyo. Yeye si yeye yule jana, leo, na hata milele, maana kamwe hakuwa zaidi ya mwanadamu. Hawezi kutimiza ahadi Yake. Yeye amethibitisha, kwa mashahidi hawa, Yeye hatimizi ahadi Yake, kwa hiyo Kitabu hicho kinapaswa kutupwa kwenye pipa la takataka na kusahau. Hakuna kitu kama hicho."

28 Sasa, kumbukeni, ninatumia sauti ya mwendesha mashtaka, kupigilia kesi yake. "Vema, Yeye alisema katika Luka 17:30, ambapo alisema, 'Katika siku za mwisho, Mwana wa Adamu atafunuliwa,' Mungu

angejifunua Mwenyewe kwa Uzao wa Ibrahimu,” kama alivyomsikia mhubiri mlokole akihubiri wakati mmoja na kusema ya kwamba Yeye angejifunua Mwenyewe tena katika wanadamu, akiitwa Mwana wa Adamu.

“Ufunuo 10, Yeye anasema ya kwamba alidai mjumbe wa malaika wa mwisho, kulingana na wakati wa kanisa katika Laodikia, ambao ulikuwa uwe vuguvugu, ya kwamba Yesu (ambaye alikuwa ni Neno) angetupwa nje ya kanisa. Yeye alidai ya kwamba katika vipindi hivi vya wakati ya kwamba kulikuwako na mambo ambayo hayakuwa yamefunuliwa wale watengenezaji katika siku za mwanzoni, lakini katika siku za mwisho, ya kwamba, mwishoni, ninii wa malaika wa saba, Ujumbe wa mjumbe wa saba, ya kwamba Maandiko haya yote yangefanywa halisi na kudhihirishwa. Hakuna mtu kama huyo duniani, hajawahi kuwako na kamwe hatakuwako,” anadai.

29 Yeye anadai ya kwamba, katika hilo, “Mungu anadai katika Biblia Yake, ya kwamba kanisa lingekuwa ni la kawaida na kuondoka mahali pake, ya kwamba katika Malaki 4 Yeye angemtuma tena nabii, ambaye amemtuma tayari, mara mbili, Eliya na Yohana Mbatizaji. Angemtuma nabii kwa ninii ... naye angekuwa katika nguvu za Eliya. Na huduma yake, matendo yake, kila kitu, ingekuwa ni Eliya. Halafu basi katika huduma yake, angewaita watu kutoka kwenye hali hii ya kawaida, wairudie ile Imani halisi ya baba wa kimitume. Na hakuna kitu kama hicho kinachoendelea.

“Na Yeye pia anadai ya kwamba mbingu na nchi zitashindwa, bali Neno Lake halitashindwa kamwe.” Naye anasema ana thibitisho hapa, alasiri ya leo, kuonyesha ya kwamba Hilo hushindwa. “Na ni nani huyu Yesu aliyefufuka katika wafu? Ninyi nyote mmepandisha msisimko katika lundo la saikolojia ya kiakili. Wala hakuna kitu kama hicho; mnategemea tumaini la uongo.”

Sasa, nafikiri hilo linatosha kwake kusema. Nafikiri ameingiza Biblia nzima. Sasa hebu aketi chini, huyu mwendesha mashtaka. Sasa hebu shahidi wa mwendesha mashtaka aketi chini pia. Wanashuka kutoka kizimbani.

30 Basi jukwaani sasa, tutamwita Shahidi wa Mshtakiwa, Roho Mtakatifu. Yeye anakuja kunena. Ninatumaini mnaona jinsi mwendesha mashtaka ameikazia kesi yake kwa Maandiko. Sasa, Shahidi wa Utetezi, ambaye ni Roho Mtakatifu, anakuja kumtetea Mshtakiwa, Neno. Nafikiri wasingeweza kumpata aliye bora zaidi.

Kwanza, Yeye anaitaka mahakama hii ijue, ya kwamba mfasiri wa Neno la Mungu, kwa watu, mwongoza mashtaka, ndiye mfasiri yule yule aliyemfasiria Hawa Neno la Mungu. Anaitaka mahakama ielewe jambo hilo, ya kwamba mfasiri huyo ndiye mfasiri wa Hawa, ambaye husema kila sehemu Yake ilikuwa ni kweli ila Neno moja tu. Naye anakutaka ujue pia ... Yeye Ndiye, kumbukeni, aliyelandika Biblia. Pia anawatakeni mjue, ya kwamba, hapo mwanzo, ya kwamba neno moja mbali na Neno la Mungu, lilisababisha mauti yote na huzuni na maradhi. Naye anawatakeni mjue ya kwamba Mungu pia alisema, katika Neno Lake, kwenye mlango wa mwisho, kama ule wa kwanza, ya kwamba, “Mtu yeyote atakayeondoa chochote kutoka Hapa, au kuweka kitu kingine chochote Kwake, ataondolewa sehemu yake kutoka katika Kitabu cha Uzima.” Haina budi kuwa ni Neno, na Hilo pekee. Anataka mahakama ijue kwamba yule aliyetilia mkazo sana haya yote, ni mfasiri wa Hawa.

31 Yeye anawatakeni hili...anaitaka mahakama hii ijue tena, huyo ni, Shahidi wa Mshtakiwa, Yeye anataka kuitazamisha mahakama hii na kuwaonyesha ya kwamba ahadi hizo ni kwa waaminio pekee; si wanaojisingizia imani, wasio na subira, ama wenye kushuku. Inabadilisha picha hiyo sivyo? Ni ninii tu ... Si kwa wale watu wanaojiita waamini; ni kwa waaminio tu, si kwa wale wanaosema wao ni waaminio. Shetani anasema yeye ni mwamini, pia, mnajua. Si kwao. Ni kwa waamini halisi tu.

Na Shahidi huyu wa Utetezi anapaswa kujua kama watu hawa ni waaminio au la, kwa sababu, hata hivyo, Shahidi wa Utetezi ndiye anaye—hulihuisha Neno Lenyewe. Yeye anajua kama unaamini ama huamini. Yeye Ndiye aliyepewa na Mungu, kulifanya litimie. Haleluya! Yeye Ndiye anayethibitisha jambo hilo. Yeye Ndiye anayelifanya litimie. Yeye Ndiye anayejua kama limeanguka mahali pazuri au la, Shahidi huyu wa Utetezi wa Neno. Shahidi wa Mshtakiwa anajua kama ndivyo ilivyo ama sivyo, Yeye Ndiye mwenye kulihuisha Neno.

32 Na tena anaielekeza mahakama hii kwenye Neno la ahadi linalozungumziwa. Yeye kamwe hakuweka wakati wowote maalum kwa mambo haya kutukia.

Mnaona jinsi wanavyoweza kukusomea Neno vibaya? Sasa watu hawa wanaosema, “Hebu nione jambo *hili* likitukia,” mnaona, hata hawalisomi Neno vizuri. Hiyo ni kusema, kama mtu huyo ni mwamini wa kweli, Yeye bado hakuweka kikomo cha wakati wo wote.

Yeye pia anataka mahakama ikumbuke ya kwamba Neno hili limeandikwa, na Yesu Kristo, Neno lililodhihirishwa, alisema, “Neno ni mbegu ambayo mpanzi alipanda.” Na mbegu hiyo inaweza tu kujizaa yenyewe, kutoa ahadi yake, kama iko katika ardhi sahihi ambayo itahuisha mbegu. Amina. Kwa namna fulani tukibadilisha kisa hicho, sivyo? Haina budi kuwa mahali panapofaa.

33 Punje ya mbegu inayokaa kwenye dawati hili kamwe haitakuza mavuno. Punje ya—ya mahindi hapa

juu, kwenye jiwe la bluu, haitafanya kitu. Mbegu ya mahindi haina budi kuanguka kwenye ardhi ambayo imerutubishwa kwa ajili ya hiyo punje ya nafaka, la sivyo haitakua.

Naye Mungu alisema ya kwamba Neno Lake ni mbegu ambayo mpanzi alipanda, nayo haina budi kuanguka katika udongo mzuri. Udongo huo ni imani. Ni mbegu, na haina budi kuanguka katika ardhi hii, la sivyo haiwezi kuhuishwa. Kwa maneno mengine, Roho Mtakatifu, Shahidi wa Mshtakiwa hapa, anasema ya kwamba hata hawezi kuijia mpaka itakapoanguka kwenye udongo mzuri. Yeye ndiye anayehiusha.

Shahidi wa Utetezi anamwita shahidi wake wa kwanza.

34 Nafikiri kama mwongoza mashtaka angeweza kuwaita mashahidi, hapa duniani, wathibitisha kwamba Neno si la kweli, nafikiri Shahidi wa Mshtakiwa ana haki ya kuwaita mashahidi wanaoweza kuthibitisha Hilo ni la kweli. Kwa sababu, swali sasa ni kati ya waaminio na wasioamini, pamoja na Neno, wakati Neno likikua.

Shahidi wa Utetezi anataka kumtambulisha kwenye mahakama hii, alasiri ya leo, shahidi wa kwanza, ni Nuhu. Nuhu alisema ya kwamba aliishi katika wakati wa kisayansi sana. Nuhu anataka kutoa ushahidi. Naye alisema aliishi katika siku ambapo watu walikuwa wameondoka kwenye miujiza na kadhalika. Na ndipo akasikia Neno la Mungu likimwambia ya kwamba atauangamiza ulimwengu kwa maji, na maji yangeshuka kutoka juu. Ingenyesha, ambapo haikuwa imenyeshwa hapo kabla. Lakini anasema ya kwamba Ne—Neno la Mungu, yeye akiwa ni nabii, Neno lilimjia, naye akaanza kuhubiri ya kwamba Neno litatimia, kwa sababu Hilo lilikuwa ni Mungu. Na pia anaitaka mahakama hii ijue ya kwamba Bw. Asiyeamini, Bw. Mwenye Kushuku, na Bw. Mkosa Subira, walimjaribu wakati wote. Lakini akiwa ni nabii, akijua ya kwamba Mungu asingeweza kusema uongo, yeye alishikilia Neno, haidhuru.

35 Wakamjia na kusema, "Sasa, Nuhu," Bw. Asiyeamini akasema, "utathibitishaje kuna mvua yoyote kule?"

"Sijui iko wapi. Lakini kama Mungu alisema hivyo, hilo—hilo latosha."

"Itanyeshaje wakati hakuna mvua kule?"

"Sijui. Lakini Mungu alisema hivyo, na hilo latosha."

Bw. Mwenye Kushuku alikuja na kusema, "Kama ingekuwa ni kitu kama mvua kushuka chini kule, basi itambidi ashuke aje hapa na kupata mvua na kuipeleka kule juu. Atafanyaje jambo hilo?"

"Sijui." "Na baada ya kuijenga safina ..."

36 Kwanza anataka kusema, ya kwamba wakati alipotoa tamshi hili, akiwa nabii miongoni mwa watu, kila mtu alimcheka, na kusema, "Sioni mvua yoyote."

Vema, wakati alipoenda kuijenga safina, walisema, "Labda baada ya safina ..." Bw.—Bw. Mkosa subira kulijaribu kumwambia, "Labda baada ya safina kujengwa, basi mvua itanyesha." Lakini wakati safina ilipokamilika, bado haikunyeshwa.

Haikunyeshwa siku iliyofuata, haikunyeshwa juma lililofuata, haikunyeshwa—haikunyeshwa mwezi uliofuata, mwaka uliofuata. Na wakati alipomaliza safina, bado haikunyeshwa.

37 Ndipo basi akasema, siku moja Sauti ya Mungu ilimrudia ikamwambia ya kwamba ataona ishara ya kimbinguni katika maumbile, ya kwamba ndege na wanyama wataingia ndani ya hii. Na halafu Bw. Asiyeamini akamcheka na kusema, "Imekuwa maskani ya ndege. Yeye alijenga kituo cha ndege, badala yake." Na wote walimcheka na kumfanyia mzaha.

Lakini, siku moja, Mungu alinena naye, na kusema, "Ingia safinani."

Ndipo Nuhu akasimama mlangoni na kusema, "Mnapata wito wenu wa mwisho. Ingieni!" Na hakuna mtu aliyeingia ila familia yake mwenyewe.

Kwa hiyo anasema aliingia katika safina. Naye akaiambia familia yake ndogo ya kupendeza, sasa, huyu ni nabii Nuhu. "Loo, katika saa nyingine, hapana shaka, mvua itakuwa ikinyesha."

Na wakati alipoingia, mlango ulijifunga kimbinguni nyuma yake. Akasema, "Unaona sasa, mpenzi," kwa mkewe, kwa wake za wanawe na wanawe, "tumefungiwa ndani pamoja na Mungu.

38 "Sasa tuna dirisha hapa. Piga hatua upesi, upesi sana. Usiikose. Kimbieni, upesi sana, na mwende juu hapa sasa. Iko karibu kunyeshwa, hapana shaka."

Na baadhi ya watu huko nje waliomsikia akihubiri, wakasema, "Sijui kama mzee huyo mshupavu wa dini angeweza kuwa sahihi?" Bw. Asiyeamini, Bw. Mwenye Kushuku, Bw. Mkosa Subira, wote walikaribia, wakasema, "Tutaona." Kasema, "Nuhu uko mle ndani?"



"Naam."

"Fungueni, tungependa kuangalia kote."

"Mungu ameufunga mlango. Siwezi kuifungua. Hakuna komeo humu ndani la kuufungulia."

Sasa wao walisema, "Maskini mzee huyo, aliingia mle na kuufunga mlango huo, na kujaribu kutufanya tufikirie ... Ni udanganyifu. Anajaribu kututisha."

39 Na kuna mashahidi wa mwendesha mashtaka, wameketi pale, wakisikiliza haya yote, kwa kuwa wana hatia ya kufanya jambo hilo. Biblia ilisema hivyo, "Wenye kudhihaki!"

"Nao wakanidhihaki, wakanifanyia mzaha.

"Na hata, mimi mwenyewe, nilikuwa nikitazamia mvua. Siku nzima, hakukuwa na mvua. Kesho yake, hakukuwa na mvua. Kesho yake, hakukuwa na mvua. Siku nne, hakuna mvua. Siku tano, hakuna mvua. Siku sita, hakuna mvua. Lakini Mungu hakuniambia wakati mvua itanyesha, Yeye alisema tu, 'Itanyesha.' Yeye hakuweka kikomo cha wakati wo wote. Yeye alisema tu, 'Itanyesha.'"

40 Kamwe hakusema, "Mara tu mtakapowawekea mikono wagonjwa, wataruka na kukimbia huku na huko sakafuni," kama vile mwenye kushuku anavyotaka kukufanya ufikiri. Yeye alisema, "Watapata afya." Kamwe hakusema ni lini, vipi. "Watapata afya!"

Yeye alisema, "Maombi ya imani yatamwoko mgonjwa," katika Yakobo 5:14, "Mungu atamwinua." Lini? Yeye hakusema. Yeye alisema tu angefanya hivyo.

Marko 16, Yeye alisema, "Uuambie mlima huu, 'ng' oka, 'wala usitie shaka moyoni mwako, bali amini ya kwamba yale uliyosema yatatimia." Yeye hakusema ni lini. Yeye alisema ingekuwa hivyo! Haleluya!

Mnaona yule mfasiri wa uongo wa Neno pale? Ndipo unasema, "Vema, hebu nikuone ukimfanya mtu huyu, amekuwa kwenye kiti cha magurudumu kwa muda mrefu. Hebu nione. Yeye anasema ana imani." Huyu ibilisi! Mnaona yeye ni nani?

Yesu kamwe hakusema wangeruka moja kwa moja juu na kuona hapo hapo. Watu wengi wa Kipentekoste wamewazia jambo lile lile, bali Biblia haikusema jambo hilo kamwe. Yeye alisema, "Kama wangeamini, wangepona." Naye ana mashahidi Wake hapa kuthibitisha jambo hilo.

Nuhu alisema, "Baada ya miaka mia moja na ishirini, ndipo mvua ikanyesha." Lakini, ilinyesha. Nuhu alijua ya kwamba ataona jambo hilo katika kizazi chake, kwa sababu alijenga safina, alikuwa tayari kuingia.

Sasa, sasa tunaona ya kwamba hiyo ilikuwa ni kweli. Sasa huyo ni Nuhu, shahidi wa kwanza.

41 Sasa, shahidi wa pili, tutamwita. Hebu tumwite Ibrahimu. Yeye alisema, "Nilikuwa nabii, nami nilitabiri chini ya uvuvio wa Mungu. Naye aliniambia ya kwamba mke wangu, akiwa na umri wa miaka sitini na mitano, na mimi sabini na mitano, katika umri huo, wakati huo, ya kwamba nitapata mtoto kwa Sara. Hata hivyo, hakika, yeye alikuwa ... Nilikuwa tasa; alikuwa, tumbo lake la uzazi lilikuwa limekufa. Alikuwa amepita wakati wa kukoma hedhi, kwa miaka ishirini, ama zaidi Nilikuwa nimeishi naye miaka hii yote, na hakukuwa na dalili ya watoto. Alikuwa, tumbo lake la uzazi lilikuwa limekufa. Na, lakini Mungu aliniambia nitampata mtoto.

"Nawe wajua, Bw. Asiyeamini, Bw. Mwenye Kushuku, na Bw. Mkosa Subira, baada ya siku ishirini na nane za kwanza, wakati hakuna kitu kilichotukia kwa Sara, walinicheka na kunifanyia mzaha. Mwaka wa kwanza, walinijia na kusema, 'Una watoto wangapi sasa?'"

42 Lakini, baada ya miaka ishirini na mitano, mtoto huyo mchanga akajitokeza. Lilitukia. Mungu hakusema, "Utapata mtoto juma lijalo, kwa Sara." " Yeye hakutaja wakati wowote. Yeye alisema angepata mtoto kwa Sara. Kamwe hakusema ni lini. Yeye alisema tu angempata.

Kwa hiyo Ibrahimu akasema, "Wala sikusita kwa ahadi hiyo, kwa kutokuamini. Bali kadiri ilivyokawia, ndivyo nilivyozidi kupata nguvu wakati wote. Na nilipoona ninazidi kuwa mnyonge kimwili, ambacho kilikuwa ndicho kizuizi cha kuja kwa mtoto huyo, badala ya kuwa dhaifu zaidi katika imani, nilipata nguvu zaidi katika imani, kwa maana nilijua ya kwamba Mungu aliweza kulitimiza Neno Lake.

"Kwa hiyo siku moja nilikuwa nimeketi, nikizungumza na Sara, ndipo Malaika wa Bwana akaja. Watu watatu, wawili wao walienda Sodoma; Mmoja alisimama karibu nami na kuzungumza nami, na kuniambia mambo yatakayotukia. Nami nilikuwa mzee na nimeinama mabegani mwangu, na ilikuwa vigumu kwa Sara kutembea huku na huko. Na, mwajua, kesho yake tu, nikaanza kuona hicho kibyongo kikitoweka mgongoni mwangu. Na nywele zangu zikaanza kuwa nyeusi, na mashavu ya Sara yakawa mekundu."

43 Sasa mnasema, "Itikadi kali, Ndugu Branham!" Hebu kidogo tu, angalia kama alifanya hivyo. Angalia,

waligeuka wakawa kijana mwanamume na mwanamke. Sasa unasema, "Loo, Ndugu Branham!" Sasa, Mungu anaficha Ujumbe Wake katikati ya mistari. Seminari haitajua hilo kamwe. Hiyo ni kweli. La, la. Ni hadithi ya mapenzi.

Mke wangu pale, huniandikia barua. Naye anasema jambo moja juu ya barua, bali naweza kusoma katikati ya mistari. Ninajua yale anayonena, kwa sababu ninampenda, ninajua tu tabia yake. Ninajua anachomaanisha. "Nimeketi hapa usiku wa leo, Billy. Watoto wako kitandani. Ninakuwazia." Loo, na— najua anachomaanisha, mnaona, mnaona, maana ninampenda.

Na kama unampenda Mungu, na Roho wa Mungu yumo ndani yako, Roho Mtakatifu Mwenyewe ndiye mfasiri wa Neno hili.

44 Angalia, walikuwa na umri mkubwa sasa, Biblia ilisema hivyo. Upesi sasa, tunafikia kikomo. Ndipo akasema, "Nikageuka kuwa kijana mwanamume. Akageuka akawa msichana."

Unasema, "Loo, Ndugu Branham!"

Sikilizeni, kusudi wapate mtoto huyo mchanga... Tumbo lake la uzazi lilikuwa limekufa; mtiririko wake wa uhai ulikuwa umekufa. Sasa kupata ... Ingembidi kumfanyia tumbo lingine la uzazi. Je, ingembidi kufanya hivyo? Halafu hawakuwa na hizi chupa wanazozingiza mdomoni mwa mtoto mchanga, kusudi mama apate kuzurura kila mahali. Siku hizo, ilibidi anyonyeshwe na mama. Kwa hiyo ili kufanya jambo hilo, vena za maziwa zilikuwa zimekauka, kwa hiyo ingembidi kufanyiza vena mpya za maziwa, na kadhalika, apate kumnyonyesha mtoto. Na jambo lingine, mwanamke mwenye umri wa miaka mia moja, aingie katika utungu wa kuzaa? Itambidi kumfanyia moyo mpya. Mnaona? Kwa hiyo hakuutia kiraka tu. Yeye alionyesha, ndani yake, kile atakachofanyia Uzao wote wa Ibrahimu, watageuka kuwa wapya, watapata mwili mpya wapate kumpokea Mwana ajaye ambaye tunamtarajia. Bado ninaamini ahadi hiyo.

Unasema, "Mwenye msimamo mkali!"

45 Vema, hebu kidogo. Angalia, walisafiri, maili mia tatu kutokea mahali walikokuwa, huko chini katika nchi ya Wafilisti, hadi Gerari. Na huko chini kulikuwako na kijana mmoja jina lake Abimeleki, yeye alikuwa mfalme, naye alikuwa akimtafuta mpenzi, na hao wasichana wote warembo wa Kifilisti. Huyu hapa anakuja maskini bibi kizee, Sara, sasa, amejifunika shali yake, na Ibrahimu. Naye Ibrahimu akasema, "Mpenzi, nataka unifadhili." Kasema, "Wewe unaonekana ni mrembo sana, wakati mfalme huyo atakapokuona, atakuchukua kuwa mke wake." Na watu walipomwona, alikuwa mrembo sana! Bibi kizee? Yeye alikuwa mrembo sana, hata, Abimeleki akamchukua awe mkewe.

Na ndipo akamtokea Abimeleki katika ndoto, na kusema, "Mumewe ni nabii Wangu. Ukimgusa, wewe ni kama mtu aliyekufa." Hiyo ni kweli?

Yeye anaonyesha pale kile atakachowafanyia watoto wote wa Ibrahimu. Kasema, "Yeye hakusema ni lini angefanya jambo hilo, bali alisema angefanya hivyo." Hilo ni sawa, rafiki, hebu lisonge mbele tu. Atalifanya kwa vyovyote vile. Yeye aliahidi jambo hilo. Sasa, lakini miaka ishirini na mitano baadaye, Sara alipata mtoto, tangu wakati wa ahadi. Neno halikusema angempata wakati gani, bali lilisema angempata.

46 Hebu na tuharakishe na mashahidi hawa sasa. Shahidi wa tatu, Musa. Yeye alisema Mungu alimpa ishara ya kufanya, kuthibitisha ya kwamba hilo lilikuwa ni Neno la wakati huo. Alichukua Neno, pamoja na ishara na Sauti, na akashuka akaenda mbele ya Mchungaji Farao. Ndipo Mchungaji Farao akasema, "A-ha, huo ni ujanja rahisi wa kichawi. Nina mtu hapa ambaye anaweza kufanya jambo lile lile." Nao walifanya hivyo. Waigaji! Akasema, "Kama nisingalikuwa nabii na kujua ya kwamba hilo lilikuwa ni Neno lililoahidiwa, ningalisema hayo hayafai kitu," maana hawa waigaji hapa nje wanafanya jambo lile lile ninalofanya." Lakini alijua ilitoka kwa Mungu, kwa hiyo akashikilia imara.

Mungu alisema angewakomboa watu nao wangekuja kwenye mlima fulani. Alitarajia labda wangerudi siku hiyo. Lakini, ilikuwa ni miaka kadhaa baadaye, bali walirudi. Walifika mlimani. Mungu alitimiza Neno Lake. Aliwapeleka kwenye nchi ya ahadi, kama alivyosema. Alikuwa ameliamini Neno la Mungu.

47 Sasa upesi sana nitampata shahidi mwingine, shahidi wa nne, ni Yoshua. Yeye alisema, "Mungu alipotupa ahadi, nasi tukaenda kwenye ..." Ni kama maili arobaini na kitu tu. "Na tulipofika Kadeshi-barnea, Musa alituma mashahidi wapate kujua kama tungeweza kuiteka au la. Na, loo, Waamaleki, na hayo majitu makubwa, na kuta ndefu," kasema, "tusingeweza kuichukua, hata kidogo, ilionekana kana kwamba."

Lakini mtu fulani alienda kule na kuleta ushuhuda fulani ya kwamba nchi hiyo ilikuwa nzuri. Kwa hiyo akasema, "Makabila mengine yote, walisema, 'Loo, hatuwezi kuichukua.'" Akasema, "Nilisimama na kuwatuliza watu, na kuwajulisha si ukubwa wa kitu kile huko nje; ilikuwa ni ahadi ya Mungu, Naye Mungu angefanya jambo hilo." Yeye alisema, "Baada ya kuwatuliza watu, Yeye hakutuchukua, kesho yake, juma lijalo. Miaka arobaini baadaye, Yeye alituchukua. Lakini Yeye hakusema ni lini angeenda kutuchukua; Yeye alisema atatuchukua, kwa hiyo tukavuka."

48 Ningetaka Isaya aje kwa muda kidogo tu. Mwangalie Isaya. Yeye alisema, "Nilikuwa nabii aliyethibitishwa miongoni mwa watu. Kila mtu aliniamini. Kutoka kwa Mfalme Uzia, kote kote, waliniamini. Nilikuwa nabii aliyethibitishwa. Yale niliyosema, Mungu aliyafanya yatimie. Yeye—Yeye alitimiza maneno yangu, niliyosema, yakatimia, kwa sababu niliyanena katika Jina Lake, Yehova." Yeye alisema, "Siku moja, Yehova alinena nami na kusema, 'Nitawapa ishara, bikira atachukua mimba.' Nami nikasema, nilinena tu kama vile Yehova alivyosema."

Kasema, "Nami ninawataka mjue ya kwamba, mahakama hii, ya kwamba kila msichana wa Kiebrania aliweka tayari vijiatu na kila kitu ampate mtoto huyu mchanga. Bikira alikuwa achukue mimba. Na likaendelea, miezi, halikutukia. Majuma, halikutukia. Yapata miaka mia nane baadaye, jambo hilo likatukia, lakini bikira alichukua mimba na kuzaa mtoto." Yehova kamwe hakumwambia lingetukia kesho, bikira fulani katika kizazi chako. Yeye alisema tu, "Bikira atachukua mimba," na hilo latosha. Yeye hakusema ni lini. Yeye alisema tu angefanya hivyo.

49 Sasa, kama inapendeza mahakama, naomba niwe shahidi Wake anayefuata? Ningetaka kumtetea, shahidi anayefuata. Ahadi ya Neno la siku hii, ndiyo ninayoishuhudia.

Wakati wa kuzaliwa, kama mvulana mdogo huko Kentucky, mnaliona kwenye kadi za maombi na kila kitu, ile Nuru ilisimama pale. Nilimwambia mama yangu na baba yangu, kote katika nyakati. Natumaini hili halisikiki binafsi, bali ninasimama tu kama shahidi mbele Zake. *Huyu* ni Yeye katika umbo la Neno. Sikujua ilimaanisha nini; hakuna mtu aliyejua. Huko nyuma kule milimani, katika umri mdogo ... Hata hatukuwa na dirisha la kioo kama ninyi nyote mlivyo nalo sasa; mlikuwa na maskini kilango kidogo ulichokisukuma ukakifungua kama dirisha. Na asubuhi hiyo, Nuru ikaingia.

Ningewaambia watu, nimwambie mama. Mambo ambayo ningemwambia, sikuzote yangetukia jinsi hiyo. Hawakuamini jambo hilo. Wakasema, "Sivyo ilivyo." Lakini yapata miaka thelathini baadaye, Mungu alilithibitisha kwa thibitisho la kisayansi, ya kwamba ilikuwa kweli. Ilikuwa hivyo, maana ni ahadi.

50 Kwenye ule mti, nikiwa na umri wa miaka saba, ambapo ile Sauti ilinena nami na kusema, "Kamwe usivute sigara, kutafuna, wala kunywa pombe, wala kuchafua mwili wako."

Na mimi katika nyumba ya wauza pombe, hata sikujua Biblia ilikuwa nini, si zaidi ya neno moja. Huenda tungeweza kupata shajara ya mwaka, bali siyo Biblia nyumbani mwetu. Hakuna kitu ila lundo la ... Si kuzungumza dhidi ya watu wangu, bali Mungu anajua yote kuhusu jambo hilo. Hakukuwa na njia hata kidogo, watu wangu waliotangulia, nyuma ya hao walikuwa Wakatoliki. Wote walikuwa wamefunga ndoa mbali na kanisa na wakaondoka, wala hakukuwa na dini hata kidogo. Hata hatukujali jambo hilo.

Lakini Yeye—Yeye aliniambia kile kingetukia, ya kwamba haikunipasa kuvuta sigara, au kunywa pombe, wala kuuchafua mwili wangu kwa njia yoyote, kungekuwako na kazi nitakayofanya nitakapokuwa mtu mzima. Vema, ilikuwa ni miaka na miaka baada ya hapo. Nilijua ninge kuwa mhudumu? Nilichukia wazo la mhubiri. Lakini ilitukia, hata hivyo. Inaonyesha ya kwamba Yeye hutimiza Neno Lake. Miaka kumi na saba baada ya Yeye kunitokea kule kichakani ...

Tunaona, kesho yake baada ya jambo hilo, Yeye alinionyesha daraja linalovuka mto, kwa mapana, likaonyesha watu kumi na sita wakianguka kutoka humo. Nikamwambia mama. Huku nimeketi kuuegemea mti, nikiangalia. Kasema, "Ulishikwa na usingizi, mpenzi."

Nikasema, "La, kamwe, mama. Niliitazama."

Miaka kumi na saba kamili tangu siku hiyo, Daraja la Manispaa huko Jeffersonville lilijengwa kuuunganisha na Kentucky, na wa saba... Na hao watu kumi na sita walipoteza maisha yao kwa jambo hilo, kama tu vile ilivyosema. Loo, vivyo hivyo Bw. Asiyeamini amenijaribu wakati wote!

51 Na hebu nimwulize tu mwendesha mashtaka huyu kipofu, kuhusu Yesu kuwa hapa na makovu ya misumari mkononi Mwake. Kamwe hakusema jambo kama hilo. Yeye alisema, wakati atakaporudi kutoka Mbinguni, ya kwamba, "Kila goti linapaswa kupigwa, na kila jicho litamwona, na kila ulimi utakiri." Yeye aliahidi tu kuzirudisha nguvu za Roho na kulithibitisha Neno Lake, la Marko, na kile ambacho angefanya. Yeye haninii tu ... Ni kwamba tu hawalipati.

52 Sasa, juu ya msingi wa mjadala huu, alasiri ya leo, nasi tukiishi... Ambapo, itanibidi kuacha, mnaniona nikigeuza kurasa hizi za fungu la maneno na kadhalika, sina budi kulielezea, lakini ninafikiri tuko karibu sana sasa kulipata.

Sasa bado wao hawataamini. Yesu aliahidi ya kwamba, "Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, na kama ilivyokuwa katika siku za Lutu, ingekuwa katika siku ya mwisho." Tunalo. Liko hapa. Tayari limethibitishwa, ni Maandiko mangapi tu! Katika wakati wa Sodoma, kile kilichompata Ibrahimu, kingeurudia tena Uzao wa kifalme wa Ibrahimu, ulio ndani ya Kristo; Kristo akirudi katika umbo la Neno, akitenda kazi katika wanadamu, na akionyesha ishara ambazo aliahidi zingeonekana, zingefanywa. Yeye aliahidi ya kwamba angefanya hivyo. Mungu aliahidi jambo hilo. Na Mungu atatimiza ahadi Yake.

53 Na sasa, miaka michache iliyopita, niliwaambia ya kwamba Yeye alinena nami na kusema, "Kutakuwa na hatua tatu za huduma hii. Na moja ya hizo itakuwa ni kuwashika watu mkono, nami ningejua shida zao zilikuwa ni nini." Ni wangapi wanaokumbuka jambo hilo? Hakika. Hivi sikuwaambia, "Kama ningekuwa mwaminifu," ya kwamba Yeye aliniambia, "ingetukia ya kwamba ningejua hata siri zilizokuwa moyoni mwao"? Je! Niliwaambia jambo hilo? Ni wangapi wanaokumbuka jambo hilo? Je! Lilitukia? Halikutukia siku iliyofuata, ilikuwa ni miaka kadhaa baadaye, bali lilitukia.

Naye alinena huko chini mtoni, akasema, "Kama vile Yohana Mbatizaji alivyotumwa kutangaza kuja kwa Kristo, mwishoni mwa huduma yake, Yesu alikuja. Na kama vile Yohana alivyotumwa, vivyo hivyo huduma yako itatangulia Kuja kwa Pili kwa Kristo." Na kumekuwa na ufufuo wa ulimwengu mzima miongoni mwa watu wa Mungu, kote ulimwenguni, katika miaka kumi na mitano iliyopita; ufufuo mrefu zaidi. Mwanahistoria ye yote anajua ya kwamba hakuna uamsho unaodumu kwa zaidi ya miaka mitatu. Na hii ni miaka kumi na mitano. Na hebu angalia kanisa leo, limepoa. Tunangojea Kuja Kwake. Yeye anajithibitisha Mwenyewe, akijionesha.

54 Sasa, mambo haya yote yametukia. Yeye aliahidi mle ndani, ya kwamba, "Ungejua siri za moyo."

Sasa hatua ya tatu ndiyo kwanza inaibuka katika huduma sasa. Sitachukua wakati kuingia mle, maana nafikiri sipaswi. Lakini wengi wenu hapa mnajua jambo hilo, mnaona, juu ya yale yaliyotukia.

55 Sasa, wakati nilipowaambia, wakati nilipokuja kwenye Jiji la Kansas hapa chini kwa mara ya kwanza, na huko chini Arkansas, kwamba mambo haya yangetukia, nayo haya hapa. Sisi ni mashahidi walio hai ya kwamba yametukia. [Sehemu tupu kwenye kanda — Mh.] ... Mungu amesema litatimia. Hakusema lingetukia papo hapo. Yeye alisema litatimia.

Marko 16 ilisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." Kama mimi si mwamini, basi kwa nini Neno hili limethibitishwa kuwa ni Kweli?

Kama ninyi si waamini, basi kwa nini Mungu aliwapa Roho Mtakatifu? Huenda mkawa na kila namna ya mathibitisho, huenda mkakimbia, mkanena kwa lugha, na mkafanya mambo kama watu walio na Roho Mtakatifu; bali kama hicho si kitu cha halisi moyoni mwako, kamwe hakitalifanya hilo Neno liishi. Lakini kama ni jambo halisi ndani mle, "mbingu na nchi zitapita, bali Neno hilo haliwezi kushindwa."

56 "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya." Na mnawaona wengine wakipona. Yeye hakusema wangepona papo hapo. Yeye alisema, "Watapona kama wangeamini."

Ni wangapi wanaosikia, hiyo ni Kweli? Ni wangapi wanaoamini ya kwamba bado Neno la Mungu ni kweli? Limefasiriwa vibaya tu kwa watu. Hivi hamwamini hilo? Limefasiriwa vibaya tu.

57 Sasa, sio huko nyuma katika siku za Luther, sio huko nyuma katika siku za Paulo, sio huko nyuma katika siku za Nuhu na mashahidi hawa wengine, sio miaka kumi na mitano iliyopita wakati nilipowaambia mambo haya yangetukia; bali ni leo hii huku Topeka, Kansas, leo hii, saa hii, dakika hii, hebu na tulialike Neno la Mungu kwenye shindano la kuamua. Yeye aliahidi jambo hili lingetukia katika siku za mwisho.

Sasa unaamini Yeye hutimiza Neno Lake? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Hana budi kulitimiza Neno Lake, kusudi awe Mungu. Hana budi kufanya hivyo. Hana budi kulitimiza Neno Lake.

58 Sasa, hivi Yeye aliahidi, "Kama ilivyokuwa katika siku za—za Sodoma, lingekuwa ni jambo lile lile katika kuja kwake Mwana wa Adamu," ya kwamba ange—angefunuliwa katika siku za mwisho kama alivyofunuliwa kwa Ibrahimu na Uzao wake huko Sodoma? Je! Yeye aliahidi jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Luka sura ya 17, kifungu cha 30, mnaweza kulisoma. Sasa, Yeye aliahidi jambo hilo. Yeye alisema lingetukia. Yesu alisema Maandiko yote hayana budi kutimizwa, yote aliyohadi.

Je! Yeye aliahidi katika Malaki 4, yale angefanya katika siku hizi za mwisho? Na mara baada ya jambo hili moto ungekuja, na kumteketeza asiyeamini, na wenye haki wangetembea juu ya majivu ya asiyeamini. Hiyo ni kweli. Vema, tuko papa hapa mlangoni.

59 Sasa, kabla tu ya gharika kuu kuja, Yeye aliahidi nini? Kabla tu ya kutoka kwa Nuhu—kwa Nuhu ... ama Musa kuja kuwatoa wana wa Israeli, ni kitu gani kilichotukia? Kabla tu ya kuja kwa Yesu, ni jambo gani lililotukia?

Yohana, hatukumleta kushuhudia. Tulikuwa naye hapa chini, bali si kama shahidi, jinsi ambavyo aliitwa atoke kwenye theolojia zote za siku hiyo, aende nyikani, kwa maana alikuwa atambue, alikuwa amtambulishie Masihi.

Vema, kama tungalishuka kwenda shuleni, kwa baba yake. Kasema, "Sasa, mimi ni rafiki mkubwa wa baba yako. Loo, alikuwa mzee mashuhuri. Ninampenda. Nami ninajua ... Sasa je, Ndugu Jones si yule Masihi? Sasa mnajua, Yohana, ndiye."

Mnaona, alijitenga. Kwenye umri wa miaka tisa, alienda nyikani, kwa kuwa yeye alikuwa mpenda nyika. Roho wa Eliya alikuwa juu yake. Na Roho wa Eliya; hakuwa Eliya, alikuwa mwanadamu; alikuwa ni Roho wa Mungu akiwa na Neno hilo katika siku hiyo. Naye akaenda nyikani. Ndipo wakati alipotoka, i—ilimbidi kumtambulisha Kristo, sio mtu mzuri, bali, "Yule utakayemwona Roho akishuka juu yake." Si yule mtu aliyekuwa mwalimu bora kuliko wote, si mtu yule aliyekuwa mtu wa thamani sana nchini siku hizo, bali, "Ambaye Roho Mtakatifu Mwenyewe alimtambulisha kama Neno." Neno Lenyewe lililitambulisha Neno.

60 Sasa Yeye aliahidi jambo hilo katika siku za mwisho. Yesu angefanya, angekuwa yeye yule jana, leo, na hata milele. Mnaamini jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.]

Sasa hebu na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo. Iweni na imani. Msitilie shaka. Aminini.

[Dada fulani ananena kwa lugha nyingine, halafu anatoa tafsiri. Sehemu tupu kwenye kanda — Mh.]  
Asante Bwana.

Vema. Yeye ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Unaamini jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.]

61 Sasa Yeye aliahidi kujitambulishaje? Katika mwanadamu, mwili wa kibinadamu, kama alivyomfanyia Ibrahimu, "Wakati Mwana wa Adamu ..." Ingekuwa ni Mwana wa Adamu, siyo—siyo—siyo—siyo Mwana wa Mungu sasa; Mwana wa Mungu katika Mwana wa Adamu. Katika Ezekieli, mlango wa 1, kifungu cha 2, Yehova alimwita Ezekieli Mwana wa Adamu, vile vile hasa Yesu alivyojiita Mwenyewe. Mnafahamu jambo hilo, kwa mafundisho ya juma hili. Sasa, mnaona, Mwana wa Adamu ni nini? Ni wa kinabii. Malaki 4 ilikuwa nini? Kuwa nabii. Mambo haya yaliyokuwa yatukie katika siku za mwisho ni yapi? Sasa, Yeye hakusema ni lini. Yeye alisema yangetukia, nayo yakatukia. Sasa, ninyi, kama Yeye angali ni Mwana wa Mungu, Mwana wa Adamu; tayari kufunuliwa katika siku za mwisho kwenye kiti cha enzi cha Daudi, kama Mwana wa Daudi. Mnaona, angalia, basi kama Yeye ... Kama hiyo ni kweli, Yeye aliahidi jambo hilo, Yeye anawajibika kwa Neno hilo. Yeye anawajibika kwa Neno hilo.

62 Sasa wewe gusa upindo wa vazi Lake kwa imani yako. Nami nimetoa madai haya. Kama ni la Mungu, litatimia; kama si la Mungu, halitatimia. Na hilo ndilo tu lililo kweli, angalia kama hili ni kweli, tuko miongoni mwa waaminio ama la. Sasa inakubidi kuwa mwamini, kama vile mimi ni mwaminio. Huna budi kuamini jambo hili kuwa ni Kweli. Kama ukiamini, litatukia. Sasa ombeni, kila mmoja wenu, amini katika njia yako mwenyewe.

Hebu na tuanzia upande mmoja, tuzingatia tu upande mmoja. Na ninii tu, nataka upande huu hapa ukutani, mahali fulani, mnaamini. Uwe na imani. Usitilie shaka. Amini tu, useme, "Bwana!"

Msiniangalie sasa, mnaona. Unaweza kuniangalia, lakini, angalia, acha imani yako iangalie zaidi ya hapo. Mnaaweza kunitazama kwa macho ya kimwili, bali mwangalieni Yeye kwa macho yenu ya imani, ya kwamba Yeye ni Neno hilo. Na—Naye ndiyo kwanza abadilishe kinyago Chake, mnaona, kutoka kile ambacho kisingeweza kuonekana kufikia kile kimetangazwa kabisa, Neno lililofanyika mwili. Iweni na imani.

63 Sasa msisogee huku na huko sasa. Iweni watulivu sana, wenye kicho. Unaweza kuzunguka-zunguka, katika dakika moja; bali uwe mtulivu kabisa, mwenye kicho.

Sasa, ni, ni nini? Ni karama. Karama si kuchukua, kama upanga, na kwenda, kupiga na kuchoma na kuvuta. Hilo silo. Karama ni kujiondoa tu njiani, ili Roho Mtakatifu aweze kufanya kazi katika mwili wa mwanadamu. Usijaribu kusema, "Utukufu kwa Mungu, nina karama! Nina karama, haleluya!" Kamwe hutaipata. Kama unajua tu jinsi ya kujiachilia!

Ni kama kuweka gia. Mnaona? Jibadilishe mwenyewe katika imani, kutoka kwenye kutokuamini, ingiza tu gia kidogo upesi huko nyuma, useme, "Vema, kwa namna fulani daima nimekuwa mwenye kushuku, bali kweli, sasa, ninaamini sasa." Sasa angalia kile kinachotukia basi. Fanya tu jambo hilo mara moja tu uone litakalotukia. Ombeni tu.

64 Nami hujaribu kujiondoa kwenye Ujumbe, kuingia kwenye karama. Karama, kwa, kusudi Neno lipate kujitambulisha kwa—kwa, kama Waebrania 4:12 isemavyo, "Pambanua, tambua siri zilizoko moyoni."

Omba kwa ajili ya shida yo yote. Omba, na useme tu, "Mungu, mimi—mimi ni mhitaji. Mtu huyo hanijui, bali mimi ni mhitaji."

Katika Jina la Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, kwa ajili ya utukufu wa Mungu, na kulingana na Neno la Mungu ambalo ndiyo kwanza nimalize kulihubiri, ninaichukua kila roho hapa ndani chini ya mamlaka yangu.

Sasa, haidhuru ni jambo gani linalotukia ... Huenda kukawa na jambo fulani litakalotukia katika dakika moja. Kuna mkosoaji anayeketi hapa, nami ninafikiri tu jambo fulani liko karibu kutukia. Mnaona? Kwa hiyo iweni tu na kicho sana. Kama kitu chochote kikivurugwa, wewe keti tu kimya. Wewe keti tu kimya kabisa, acha mtu huyo afanye kile wanachotaka kufanya. Angalia kinachotukia. Hebu na wasogee, na uone kitakachotukia. Mtaona kama Yeye ni Mungu au la. Mnapaswa kumwona vitani. Mmemwona katika

uponyaji; mwangalie katika vita. Shetani anajaribu awezavyo kufanya jambo hilo. Lakini hebu—hebu acha tu afanye hivyo mara moja, angalia kinachotukia.

65 Kuna mtu mwingine anayeketi hapa ambaye amekuwa akiteseka, ameketi papa hapa chini, mwanamume na mkewe. Yeye anaomba. Yeye anamwomba. Ni ugonjwa wa neva, neva usoni. Yeye kwa namna fulani ni mwanamke mnene. Mumewe amevaa shati jeupe. Yeye anaweka mikono yake juu yake. Hiyo ni kweli. Inua mkono wako, kama hiyo ni kweli, kama hilo ndilo unaloombea. Usijali. Litakoma. Ni ahadi, kama ungeamini. Uligusa vazi Lake.

Kuna bibi anayeketi papa hapa nyuma upande huu, anaugua ugonjwa wa kike. Natumaini ninii yake ... Ee Mungu! Bibi Reed, unajua sikujui. Lakini hiyo ni kweli, sivyo? Ulikuwa ukiomba, "Bwana, unirehemu." Amekurehemu. Utakuacha sasa. Wewe amini tu kwa moyo wako wote. Msitie shaka. Una imani.

66 Hapa, huyu hapa mama anayeketi papa hapa mwishoni, amevaa kofia ndogo inayoonekana ni nyeusi. Yeye anaomba kuhusu ... Ni shida. Ana shida. Hivi hamwoni ile Nuru ikining'inia pale? Mnaona? Ameinamisha kichwa chake. Ana shida ya magoti yake. Aliumiza magoti yake. Alianguka na kuumiza magoti yake. Mnaona? Simjui; Mungu anajua jambo hilo. Lakini hiyo ni kweli, sivyo, mama?

Hapa, weka mkono wako juu ya mama huyo mwingine anayeketi karibu nawe; ije moja kwa moja mpaka kwake. Yeye anaugua ugonjwa wa wasiwasi. Na hali hiyo ya wasiwasi ina ... Ana shida ya macho. Na macho yalifanyiwa upasuaji, ambao ulisababisha hilo. Hiyo ni kweli, sivyo? Inua mkono wako. Kama unaweza kuamini!

Huyu mama mwingine aliinua mkono wake papo hapo kando yake, kidogo lilimchangamsha sana. Lakini sababu, kama utaninii ... Unaamini ya kwamba Mungu anaweza kuniambia shida yako ni nini? Iko katika vifundo vyako. Kama hiyo ni kweli, pungu mkono wako namna *hiyo*. Vema.

Yeye alisema angefanya nini? "Ni yeye yule jana, leo, na hata milele." Unaamini jambo hilo?

67 Huyu hapa mtu ameketi mbele yangu. Anaumwa na yabisi kavu. Yeye kweli ... Sijui kama ataupata ama hataupata. Yeye kwa namna fulani ni mtu karibu na umri wangu. Anaugua yabisi kavu. Yeye hatoki hapa. Yeye anatoka Kansas City. Je! Unaamini ya kwamba Mungu atakuponya? Unaamini Mungu anaweza kuniambia jina lako ni nani? Bw. Francis Wewe amini kwa moyo wako wote. Yeye alikuwa akijaribu kukunyang'anya huo, bwana. Na yeye—yeye ... Ulikuwa unafikiri nilikuwa nikimaanisha mtu mwingine, bali ilikuwa ni wewe. Ndipo wakati niliposema hilo, hisi ya ajabu kweli ilikuja juu yako, tamu sana na motomoto. Kama hiyo ni kweli, pungu mkono wako namna *hii*.

Pia, mke wako anayeketi pale, yeye ni Bibi Francis. Anaugua pia yabisi kavu. Naye ana shida ya macho yake, na shida ya masikio yake. Hiyo ni kweli? Hiyo ni kweli.

68 Yule bibiye anayeketi karibu na yeye, papo hapo karibu na yeye hapo, anaumwa na vena zilizovimba. Sawa. Ana kasoro fulani ndani, namna fulani ya... Ni shida ya kibofu. Ana shida ya kibofu. Yeye pia anatoka Kansas City. Bibi Gregg Hiyo ni kweli.

Kama mimi sifahamiani kabisa nanyi watu, inueni mikono yenu namna *hiyo*, ili kwamba, ninamaanisha, kwa hawa watu hapa walioitwa, inueni mikono yenu, ninyi watu ambao mmeitwa sasa hivi, kama hatufahamiani.

Ni kitu gani? Mungu yule yule aliyeshuka katika mwili wa kibinadamu, na kula nyama na kunywa maziwa. Naye Yesu akasema ... Naye Ibrahimu akasema, hasa, ya kwamba Yeye alikuwa "Elohimu," Mungu aliyedhihirishwa katika mwili. Yesu alisema, "Kama ilivyokuwa katika siku hiyo, ambapo Yehova, Mwana wa Adamu tena, katika mfano wa kinabii, kama alivyokuwa, angerudi tena katika siku za mwisho," kabla tu miili yenu haijabadilishwa. Sisi, hatungeweza ... Mnaona, Sara asingeweza kumpokea mtoto huyo katika mwili huo, sivyo? Ibrahimu asingeweza, katika mwili wake. Mwili wake ulipaswa kubadilishwa. Vivyo hivyo na sisi pia, kumpokea Mwana. Chukua Neno, Naye ni Mwana. Ni Neno. Mnaamini jambo hilo?

Sasa inamisheni vichwa vyenu kwa muda kidogo.

69 Kabisa, kwa moyo wako wote, je, Mungu ana haki ya kufanya ahadi hizi? Unaamini Neno Lake ni Kweli? Je! Mnaamini ya kwamba mashahidi hawa ni mashahidi wa uongo tu, kwamba hawakuwa na imani ya kuliadini hapo mwanzo? Ninyi ndinyi wazee wa mahakamani na ninyi ndio hakimumu. Kila wazee wa mahakama hawana budi kuamua, hakimumu hana budi kutoa hukumu. Umefanya uamuzi wako kwamba Neno la Mungu, la Marko 16, ni Kweli? Kama umeamua, inua mkono wako. Nimewaleta mashahidi jukwaani, waliokuja kwa njia ile ile kama hii katika siku za mwisho, na kuthibitisha ya kwamba Neno la Mungu lilikuwa ni kweli. Na Neno la Mungu linaahidi jambo hili katika siku za mwisho. Nami nipo hapa, nanyi mpo hapa, mbele zenu, kuthibitisha hayo mengine, kila mmoja wenu. Kila mmoja wenu angeweza kuitwa, mmoja mmoja, namna hiyo, kama mnaamini. Waulize watu hawa, zungumza nao, ambapo Roho Mtakatifu ameita.

70 “Unafanya nini sasa, Ndugu Branham?” Ninajaribu kuondoka Kwake. Linaendelea kutendeka kila mahali jengoni; unaiona tu ikimulika.

Mnaona, pamoja na hayo, ninajaribu kuwafanya mliamini. Iweni na imani na Mungu. Aminini hilo. Yeye ana haki ya kuandika haya. Yeye amelithibitisha, na kuhakikisha ya kwamba ni Kweli. Yeye alitabiri jambo hilo, miaka thelathini iliyopita, na kulithibitisha leo. Yeye alisema jambo hilo, miaka elfu mbili iliyopita, na kulithibitisha leo. Neno Lake ni Kweli. Na kila Neno la Mungu lina pumzi, na lote ni Kweli. Na Marko 16 ilisema, “Wataweka mikono yao juu ya wagonjwa nao watapata afya.”

Baraza la wazee, uamuzi wenu ni nini katika mahakama hii alasiri ya leo? Je! Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele? Inua mkono wako. [Kusanyiko linasema, “Amina.” — Mh.] Je! Mmeshawishika kabisa ya kwamba Marko 16 ni Kweli, Neno la Yesu Kristo, “Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya”? Inueni mikono yenu. [“Amina.”]

Basi, Shetani, huna budi kuondoka. Bw.Asiyeamini, huna shughuli kati yetu tena. Bw.Mwenye Kushuku, ama Bw.Mkosa Subira, sijali itachukua muda gani, itatukia.

71 Je! Mnaniita mimi mwaminio? Inua mkono wako kama unaniita hivyo. Mimi ni mwamini. Nitawaombea, niwawekee mikono. Je! Mnaamini ya kwamba wachungaji wenu hapa ni waaminio? Inueni mikono yenu. Ni wahudumu wangapi wanaoamini huko nje? Inueni mikono yenu.

Nitawaomba wahudumu wanaoamini waje hapa kwa dakika moja. Hiyo ni sawa, mchungaji? Kamilifu. Ninataka kila mhudumu katika jengo hili, ambaye ni mwamini, aje hapa na asimame pamoja nami kwa muda kidogo tu. Ninataka waaminio halisi sasa. Kumbuka, hatutaki waamini wa kujifanya. Tunataka waamini halisi. Njoo hapa na usimame jukwaani. Mtaona jambo fulani likitukia sasa. “Ninaamini uliniambia Ukweli.”

72 Sasa kumbukeni, kimya kabisa kwa dakika moja, wakati wahudumu hawa wanapokuja, ninataka kuwaambia jambo fulani. Sasa ni nini, itakuwaje? Tendo lako, kutokana na tendo lako ... Mtu fulani aliteleza. Ni sawa. Tendo lako, tangu wakati huu na kuendelea, litakuwa uamuzi wako. Ni wangapi wanaoamini jambo hilo, inua mkono wako.

Sasa kila mtu aliye na—aliye na kadi ya—ya maombi, simameni upande wa mkono wa kulia hapa, njoni upande *huu*. Ninyi, kila mmoja wenu katika marefu yenu, simameni katika mkono wa kulia wa marefu yenu, katika mkono wa kulia wa marefu yenu.

Sasa hao upande wa pili kule, itwabidi waje huku. Vema.

Wote hawa upande *huu*, wenye kadi za maombi, simameni katika marefu *haya*; namna hii, upande wa kulia. Huo ungekuwa upande wa kushoto. Samahani. Upande *huu* hapa ungekuwa mkono wako wa kulia. Huo ni upande wako wa kushoto. Sasa njoni moja kwa moja namna hiyo, tengenezeni mstari wenu.

Sasa ninyi wahudumu wote njoo hapa na kufanya mistari miwili, moja kwa moja upande *huu*, mistari miwili moja kwa moja upande *huu*; papa hapa na papa *hapa*, kila mmoja wenu.

73 Sasa ni wangapi wenu wanaoamini? Inua mkono wako, useme, “Sasa tena ninataka kumwonyesha Mungu ya kwamba ninaamini kabisa ya kwamba Marko 16 ni Kweli,” inua mkono wako. “Sasa ninalikubali.”

Ni wangapi huko nje ambao hawatakuwa kwenye mstari wa maombi, watakaokuwa wakiwaombea hawa walio kwenye mstari wa maombi, na kundi letu lote pamoja litakuwa linaomba kama waaminio? Inua mkono wako.

Sasa hebu na tuombe.

74 Bwana Yesu, Wewe ni Mungu. Wewe ndiwe “MIMI NIKO,” si “Nilikuwa,” ama “Nitakuwa.” Wewe ni “MIMI NIKO,” wakati uliopo. Hakuna nguvu zinazoweza kukuzuia. Wewe ni Mungu, na hakuna aliye kama Wewe. Unafanya Maneno Yako kuthibitishwa. Umetuhakikishia jambo hilo, kupitia kwa mashahidi alasiri ya leo katika kesi hii; baraza hili la mahakama, na pia mahakama hii, na mahakimu watakaokuwapo.

Tumefanya kesi, ya haki. Tulichukua yale aliyosema adui. Tumechukua yale aliyosema mwendesha mashtaka. Tumechukua yale mashahidi wake waliyosema. Tuliyaarudisha pamoja na ushahidi wa Shahidi wa Mshtakiwa, Naye amethibitisha ya kwamba Mungu ana haki ya kutoa matamshi haya, kwa sababu Yeye huyatimiza, kwa mwamini, kwa mashahidi wengi zaidi kuliko asiyeamini anavyoweza kutoa mashahidi. Sasa tunajua ya kwamba hiyo ni kweli. Inategemea tu kama watu wamelipata kuwa ni kweli, Neno la Mungu kuwa ni Kweli.

75 Tujalie, Bwana, ya kwamba kila mtu anayepitia kwenye mistari hii hapa ... Baba, watu hawa wanaosimama hapa. Baada ya mimi kuondoka, mtu fulani anaweza kusema Ndugu Branham aliwawekea mikono, lakini nataka watu wajue ya kwamba wachungaji hawa wana haki ya kuwawekea wagonjwa mikono kama mtu ye yote anavyo. Haiwabidi kungojea mpaka mwinjilisti fulani wa wakati maalum

atakapokuja, bali mchungaji wao mwenyewe ana haki ya kuwawekea mikono. Mungu, jalia hilo, kila mtu anayepitia kwenye mstari huu wa mikono hapa leo; ambao wameitwa na kuwekwa wakfu na Mungu, kuwawekea mikono wagonjwa.

Tunajua hatuna mikono mitakatifu, bali hatujiangalii wenyewe. Tunaangalia dhabihu yetu, Yesu Kristo, yeye yule jana, leo, na hata milele, Ambaye anatokwa na damu mbele ya kiti cha enzi cha Mungu sasa, kutusafisha, kutekeleza agizo Lake. Tujalie, Bwana, ya kwamba kila mwanamume, mwanamke, mvulana, ama msichana, anayepitia hapa, atatoka kwenye jukwaa hili, akifurahi, sawa tu na kana kwamba kwa kawaida walikuwa wazima na wenye afya. Jalia hilo. Jalia maamuzi ya wazee hawa wa mahakama, wanayodai yalikuwa, Yeye alihesabiwa haki, na jalia sasa hukumu watakayoitoa iwe ndiyo matendo yao tangu sasa. Tusaidie, Mungu, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

76 Ndugu Roy Borders ama kiongozi fulani wa nyimbo, kama utakuja hapa kwa muda kidogo tu na kuongoza. Sasa huku macho yenu yamefumbwa.

Sasa angalieni tu mstarini, wakati mstari wenu unapokuja. Njoo hapa. Tuliomba, kila mmoja wa watu hawa. Kwa nini niliwaweka hapa, ilikuwa ni hii. Sasa ninyi hapa itawabidi kushuka kuja upande huu na kuambatana moja kwa moja na hawa, pamoja na hawa hapa, wanapotoka, mnaona. Sawa. Sasa ngojeni tu mpaka wao ... Ngojeni mpaka watakapoondoka. Ngoja mpaka mstari *huu* utakapotoka; halafu wewe, mama. Papa hapa, dada, ngoja papo hapo. Mnaona, ngojeni papo hapo, mnaona. Wahudumu, baadhi yenu mnawasaidia pale, mnaona. Mnaona, huna budi kuacha mistari *hii* itoke, mistari *hii* itoke, na mstari *huu* uifuate, unaona, ukipitia.

Sasa kama unakuja hapa kwa kudhania tu, kubashiri tu, kaa nje ya mstari; huenda likakufanya kuwa mbaya zaidi. Lakini kama ukipitia hapa, ukiamini, hakuna kitu kitakachouondoa kwako. Ni wangapi wanaojua kwamba kutoka kwenye huu, huu ndio wakati wa kuamua? Ninyi mlio kwenye mstari, semeni, "Hili ndilo. Ninaamini jambo hilo. Hakuna tena kulalamika juu yake. Imekwisha, sasa hivi. Nimelikubali Neno la Mungu." Usipofanya hivyo, usiingie mstarini, sasa. Amini kwa moyo wako wote, ndipo uje.

77 Mungu amejithibitisha Mwenyewe kwa Neno, na kwa shahidi na shtaka, yupo sasa hivi, "yeye yule jana, leo, na hata milele." Hakuna kilichosalia ila kuweka mikono juu ya wagonjwa, nao watapata afya. Hawa hapa wachungaji wenu. Mnajua wao ni waaminio. Wao ni wachungaji wenu.

Nami sitaki mfikirie kwamba mimi, Oral Roberts, ama mtu mwingine, ndiye mtu pekee aliyechaguliwa kufanya jambo hili. Kila mhudumu amechaguliwa kufanya jambo hilo. Kila mwamini, kama yeye ni mhudumu, au la, amechaguliwa kufanya hivyo. Kila mtu anayeamini, ana haki ya kuwawekea wagonjwa mikono, nao watapata afya.

78 Sisemi mchungaji wenu ama mtu ye yote angekuwa akichukua karama ya utambuzi. Si lazima wafanye hivyo; huo si wito wao. Huo si wito wao, kufanya hivyo. Hiyo itakuwa mtu mmoja kwa wakati mmoja.

Lakini—lakini tunaona, ya kwamba umeitwa, kama mwaminio. "Ishara hizi zitafuatana nao," hazionyeshi mtu ye yote, "hao waaminio." Unaamini kwa moyo wako wote sasa.

Ndugu Roy, wewe ongoza wimbo, Amini Tu. Kila mtu katika maombi. Wahudumu, wanapopita hapa, wawekeeni mikono. Nanyi washirika na marafiki, mnapopitia hapa, msiwe na shaka hata moja niani mwenu; pitieni tu moja kwa moja mstarini, mkitokea hapa, msemi, "Imekwisha."

79 Sasa kumbukeni, mmekuwa mahakamani kwenye kesi hii. Uliinua mkono wako kwamba ulikuwa na uamuzi wako. Kila mtu anayeelewa, aseme, "amina." [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Umekuwa na uamuzi wako. Sasa yale mtakayofanya baadaye yatathibitisha kama mlisema kweli ama hamkusema. Hu— hukumu yako itapitishwa kwa yale ufanyayo tangu sasa. Hiyo itakuwa hivyo. Utakuwa hakimu na mzee wa mahakama. Kama kweli unaamini, halina budi kutukia. Kama unajifanya wa kuamini, halitatukia.

Maana, linathibitishwa kwa Neno, kwa Uwepo wa Mungu, kwa kila kitu kilichopo. Kuna jambo lolote lililosalia kufanywa? Kama angekuja papa hapa, alasiri ya leo, angeweza kukuponya? La, la. Tayari amefanya jambo hilo. Mnaona? Yeye ni yote... Hakuna kitu kilichosalia kufanywa *sasa*. Yeye amejithibitisha Mwenyewe hapa, kwa Neno, akathibitisha kila kitu. Jambo pekee unalopaswa kufanya ... Umeamua, umesikia kesi, umepitisha uamuzi, sasa njoo uonyeshe hukumu yako. Amina. Mungu akubariki.

Vema. [Ndugu Borders anaanza kuongoza kusanyiko katika kuimba *Amini Tu* — Mh.]

Iweni na maombi sasa, ndugu. Na hebu kila mmoja wa mabawabu awaache watu wapitie. Simama karibu kidogo sasa. Kila mtu anamgusa mtoto huyo, mguse kila mtu. Kila mtu awaguse hao watu, kwa imani sasa. Funga macho yako. [Ndugu Branham na wahudumu wanaomba na kuweka mikono yao juu ya watu. Sehemu tupu kwenye kanda — Mh.]

Amini tu,

Yote yatendeka, amini tu;



Amini tu, amini tu,  
Yote yatendeka, amini tu.

80 Sasa je! Waweza kuuimba hivi, "Sasa naamini, sasa hivi naamini"? Umeamini? Inua mkono wako, useme, "Kwa kweli ninaamini." "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio!"

Yote yatendeka, sasa naamini;  
Loo, sasa naamini, sasa naamini,  
Yote yatendeka, sasa ninaamini.

81 Wakati fulani uliopita, yapata miaka kumi na mitano iliyopita, ninakumbuka usiku mmoja nikiitwa hospitalini, kwa mvulana aliyekuwa akifa kwa dondakoo nyeusi. Kulikuwako na...moyo ulikuwa umemharibikia. Naye baba yake akaendelea kuja mkutanoni, ku—kuniita nikamwombee mvulana huyo. Naye mvulana huyo alikuwa na umri wa kama miaka kumi na mitano, kumi na sita. Nami nilikuwa na shughuli nyingi sana, nisingeweza kufanya hivyo. Na hatimaye ... Kama—kama—kama—kama ukilipeleka kwa mmoja, na huyo mwingine pia, mwajua. Kwa hiyo baba aliendelea tu kushikilia, akingojea mpaka wakati ule. Hatimaye, usiku mmoja baada ya ibada, nilienda hospitalini. Vema, daktari aliniambia ya kwamba nisingeweza kuingia. Akasema, "Kwa sababu, m—mvulana huyo ana dondakoo, nawe ni mtu aliyepoa wala huwezi kuingia na kukichukua kijidudu hicho."

82 Vema, nilimwuliza, "Tafadhali naomba niingie." Mtu huyo alikuwa Mkatoliki. Nami nikasema, nikasema, "Je! Wewe ni Mkristo?"

Akasema, "Mimi ni Mkatoliki."

Nikasema, "Kama kasisi alikuwa amesimama hapa na kujaribu kuleta—kuleta taratibu za mwisho za kanisa kwa mvulana huyo, je! Ungekubali jambo hilo?"

Akasema, "Hiyo ni tofauti. Huyo ni kuhani. Wewe ni mwanamume aliyepoa."

Nikasema, "Vipi kama nikitia sahihi karatasi, nijitwike jukumu lote?"

Akasema, "Siwezi kufanya hivyo, bwana."

Nami nikasema, "Tafadhali." Nilisema hili, "Mimi ni kama hao watu kama kasisi alivyokuwa kwako."

Hatimaye, akanivisha kama Ku Klux Klan, na vitu hivyo vyote vyeupe, na kuniingiza ndani, nami nikamwendea yule mvulana. Alikuwa amepoteza fahamu, siku mbili ama tatu. Moyo wake ulikuwa ukipiga tu kwa shida. Nimesahau upumuaji ulikuwa vipi; mdogo sana, ukipiga, kwa shida sana. Na maskini baba na mama walikuwa wamesimama pale.

83 Nami nikapiga magoti tu, na kuomba dua rahisi tu, nikamwekea mikono, nikasema, "Bwana Yesu ..." Nilitumia Andiko hili. "Ulisema, 'Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.' Hawa hapa baba na mama, wasingeng'ang'ania na kunishikilia mimi kumwekea mikono mvulana huyo kama isingalikuwa kwamba waliamini jambo hilo. Na, Bwana, nisingekuja hapa kama dhahaka. Ninaamini ya kwamba yale niliyosema na kufundisha ni Kweli." Nami nikasema, "Ninambariki mvulana huyo mdogo, katika Jina la Yesu Kristo; mwache aishi."

84 Na wakati nilipoinuka, baba na mama wa kale wakaanza kukumbatiana, na kusema, "Si ni ajabu, mama! Si ni ajabu sana!" Mvulana huyo hakuwa amebadilika hata kidogo; amelala tu pale. Nami ni—niliwaangalia.

Na maskini nesi yule aliyekuwa amesimama pale, alikuwa ni nesi maalum, mhitimu, naye alikuwa pale akimwangukia mvulana huyo. Naye akamwambia yule mama, akasema, "Unawezaje kutenda hivyo, na ujue mvulana wako anakufa?"

Na yule baba mzee, kama vile alivyokuwa karibu, loo, nadhani, alikuwa na umri wa miaka hamsini na minane, sitini, aliweka mikono yake juu ya mabega yake, kama vile baba mzee angefanya. Akasema, "Mwanangu," akasema, "huyo mvulana hafi," akasema.

"Bwana," kasema, sijui hii ilikuwa ni nini, namna fulani ya kadiogramu ama chochote kile, kasema, "upumuaji wa—wake umeshuka sana, na kwa ugonjwa huu, haijulikani katika historia, kama kamwe ukifikia katika hali hiyo, kupata kurudi tena."

85 Ndipo maskini mzee huyo akayapangusa macho yake, akamwangukia. Sitasahau jambo hili kamwe. Akasema, "Mpenzi, unaangalia chati. Hivyo ndivyo ulivyofundishwa kuangalia. Ninaangalia ahadi ambayo Mungu alitoa. 'Wataweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya.'" Mvulana huyo amepoa na ana watoto watatu, mmishenari huko Afrika. Inategemea unaangalia nini.

Sasa huenda kukawa na wengine hapa, waliofika hapa, ambao hawakupata kadi ya maombi. Nilimuuliza mwanangu pale chini. Akasema, "Hakuna shaka ila kuna wengi huko nyuma, baba, ambao

hawakupata kadi ya maombi.”

Ni waaminio wangapi walio hapa basi? Inueni mikono yenu. Je! Mtafanya jambo hili tunapoimba, “Sasa naamini”? Sasa Mungu alikuwa mwema kwako. Hutaafanya hivyo, kama mwaminio ... Haileti tofauti yoyote ni mikono ya nani, mradi tu ni mwaminio. Mnaona? Je! Mnaweza tu kuwekeana mikono, nasi tutaimba wimbo huu pamoja, “Sasa ninaamini.” Na mpaka nitakapokutana nanyi, Mungu awe pamoja nanyi!

Sasa naamini,

Hiyo ni kweli, weka mikono yako juu ya mtu aliye karibu nawe.

Sasa naamini,

Mambo yote (haidhuru kuna shida gani, mambo yote yanawezekana) yanaweze- ...

(Katika Jina la Yesu, wabariki hawa.)

Sasa naamini, loo, sasa ... (“Sasa sichezi. La, hili, sasa naamini.”

Mambo yote yanawezekana, loo, sasa naamini.

86 Sasa wote mnaoliamini, inueni mikono yenu juu namna *hiii*, “Sasa ninaliamini.” Mungu awabariki.

Hata tuonane! ... tuonane!

Hata tuonane miguuni pa Yesu; hata tuonane!

Hata tuonane; hata tuonane!

Mungu awe pamoja nanyi hata tuonanapo tena!

Sasa huku vichwa vyetu vimeinamishwa.

Hata tu ...

Mungu awe pamoja nanyi, hakika, ayapige mawimbi ya mauti yanayotisha mbele yenu, awapeleke kutoka ushindi hadi ushindi. Siku moja, miili yetu na ibadilishwe na ifanywe kama mwili Wake Mwenyewe wenye utukufu, ambapo hatutawaombea wagonjwa tena. Mpaka wakati huo, Mungu na awe pamoja nanyi, hata tutakapokutana. [Ndugu Branham anavumisha—Mh.]

Hata tuonane!

Mungu awe pamoja nanyi hata tuonanapo tena!

Sasa hebu na tuinamishwe vichwa vyetu kwa ajili ya maombi ya kufunga. Ni nani atakayeomba? [Mtu fulani anasema, “Ndugu Gibson. Ndugu Gibson.” — Mh.] Ndugu Gibson sasa, wakati tumeinamisha vichwa vyetu.



[www.messagehub.info](http://www.messagehub.info)

Mahubiri Na

**William Marrion Branham**

"... katika siku za sauti ..." Ufu. 10:7